

WAEBRANIA, MLANGO WA SABA ²



Awabariki! Nafikiri, kwanza, tuna mtoto mchanga hapa, Doc aliniambia dakika chache tu zilizopita, ndugu yangu, ndugu wa kuzaliwa, ambaye alitaka . . . alikuwa awekwe wakfu. Na sasa kama hao akina mama walio na watoto wao wachanga ambao wanataka kuwaweka wakfu kwa Bwana, tutafurahia kuwapokea sasa hivi. Na waje, wawalete watoto wao wachanga huku.

²³⁹ Sasa, na watu wengi, wao, kitu chochote wanachoita, kuwabatiza. Kanisa la Kimethodisti hufanya hivyo, na ninaamini la Kinazarayo. Sina hakika. La. Nafikiri hilo ndilo lililowatenganisha, ilikuwa ni ubatizo wa watoto wachanga, Wanazarayo na Wamethodisti Huru. Lakini, hata hivyo, baadhi yao, wanafanya jambo moja na lingine. Lakini, na baadhi yao wanawamwagia maji kidogo juu yao. Wengine wanawanyunyizia. Na, lakini sisi daima tunajaribu kuwa karibu kabisa na Biblia jinsi vile tujuavyo. Sasa, hakuna Andiko katika Biblia kwa mtoto mchanga kunyunyiziwa, wala hakuna Andiko katika Biblia kwa mtu ye yote kunyunyiziwa. Si jambo la Kimaandiko. Ni utaratibu wa kanisa Katoliki.

²⁴⁰ Lakini wao—lakini wao wanafanya jambo hilo, walileta . . . Hasa waliwaleta watoto wadogo kwa Yesu. Na—na sisi tunapaswa kumwakilisha. Tunataka kufanya jambo lile lile alilofanya Yeye. Aliweka mikono Yake juu yao na—na kuwabariki, na kusema, “Waacheni watoto wadogo waje kwangu, wala msiwazuie, kwa maana walio mfano wa hao Ufalme wa Mbinguni ni wao.” Na hivyo ndivyo tunavyoendelea kufanya hapa maskanini, tunapojaribu kuiendeleza Biblia halisi, jinsi ilivyowekwa wakfu, vizuri kabisa tujuavyo.

²⁴¹ Kwa hiyo sasa, kama mama huyo, ama mama wo wote walio na watoto wao wa kuwekwa wakfu, wakati Dada Gertie anapopiga *Waleteni*, ahaa, waleteni huku madhabahuni. Mimi pamoja na ndugu tutashuka tuje na kuwaweka hao watoto wadogo wakfu kwa Bwana. Vema.

Ndugu Neville. [Ndugu Branham na Ndugu Neville wanawaweka wototo wadogo wakfu. Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.]

²⁴² Asante, Dada Gertie. Huo ni mzuri sana. Ni wangapi wanaowapenda watoto wadogo? Kama huwapendi, una kasoro, kuna kasoro.

²⁴³ Sasa, usiku wa leo, sasa kuingia katika ibada zingine. Sisi . . . sababu ya mimi kushuka nikaja usiku wa leo. Kwa kawaida kwenye siku hizi wakati tuna ibada za uponyaji, ninafanya kama ibada moja tu kwa siku, kwa maana inanitikisa sana. Kamwe

hamtajua jambo hilo. Na hapa nyumbani ni mbaya zaidi mara mbili kuliko kwingine kote.

²⁴⁴ Nami nilikuwa nikiomba msamaha kwa kufanya kosa la kijinga kama nililofanya asubuhi ya leo. Lakini jambo la kwanza lililolifadhaisha, lilikuwa ni wakati Billy alipokuja kuniambia ya kwamba asingeweza kupata watu wa kutosha kuwapa kadi za maombi. Yeye aliweza tu kusambaza kumi na mbili ama kumi na nne. Naye alikuwa na . . . Hakuna mtu aliyetaka kadi za maombi. Nadhani kila kitu kilikuwa ni sawa. Kwa hiyo basi, kwa jambo hilo, kamwe sikuwazia. . . Na ndipo wakati nilipoanza kuita kadi hizo za maombi, nilidhani ningewapata wote kumi ama kumi na wawili, ama wo wote waliokuwa hapa ndani. Niliwaita. Nilifikia kwenye namba fulani, kitu fulani, wala hakukuwa na jibu. Tena nikaita. Hakuna jibu. Wala sikuliwazia jambo hilo hata kidogo mpaka Bibi Woods aliponiita. Akasema, “Ndugu Branham, Billy huzichukua hizo kadi na kuzichanganya pamoja, kisha anazisambaza tu. Huenda alikuwa na hiyo namba tatu,” (je! sivyo ilivyokuwa?) “namba tatu mfukoni mwake.”

²⁴⁵ Hakika, yeye kwa kawaida husambaza zote hamsini. Anapozileta mbele ya watu, yeye huzichanganya tu. Kwa hiyo kila mtu. . . Si eti kusema, “Nipe namba moja.” Hiyo ni kusema, huenda tusianzie na namba moja. Huenda tukaanza na namba hamsini, hujui, kisha turudi nyuma. Huenda tukaanza na nane na kuendelea. Huenda tukaanza na ishirini na kuendelea. Hatujui. Lakini yeye huzichanganya tu na kuzisambaza kwa watu kadiri wanavyozitaka. Na bila kufikiria haya asubuhi ya leo, huenda niliita nne ama tano zaidi, nao wasingekuwamo humo, maana huenda ilikuwa ni huko mbali sana kwenye ishirini ama thelathini mahali fulani, unaona. Na, basi, bali Bwana alitatuja jambo hilo, lakini haina pre—presha hasa kwenye hilo, kama inavyokuwa nikiwa mbali na nyumbani. Huenda nisilijaribu—nisilijaribu tena.

²⁴⁶ Lakini, hapa si muda mrefu uliopita, nilimwomba Bwana kama atatupa mkutano mzuri, ambapo niliahidi ya kwamba ni—nisingemwomba jambo hilo tena, kwa kuwa limekuwa ni jambo gumu sana. Na ni kinyume cha Maandiko. Unaona? Na kama mkininii. . . Hilo ndilo linalolifanya kuwa gumu kwangu. Kwa sababu, nikijua ya kwamba, inanifanya ni—nivunjike moyo, kwa kuanzia. Unaona? Nimevunjika moyo, kwa kuanzia.

²⁴⁷ Hata hivyo, mtu fulani alimwita mtu fulani alasiri ya leo. Bibi Woods aliitwa na mtu fulani. Na akasema, ya kwamba, “Mtu fulani kanisani aliitwa asubuhi ya leo, kuhusu mtu aliyekuwa ni mahtuti, mahtuti sana, aliyemjia Kristo alasiri ya leo, baadaye.” Ya kwamba yule—yule mtu aliyekuwa taabani alimjia Kristo.

²⁴⁸ Na jambo lingine, Bibi Woods aliniambia ya kwamba nilizungumza na dada yake, dada mkubwa, ya kwamba kweli nilikuwa nyumbani kwake hivi majuzi na nikala chakula

cha usiku pamoja naye, ama mlo wa usiku pamoja naye, huko Kentucky. Na Mwenyezi Mungu anajua ya kwamba sikumtambua mwanamke huyo. Unaona? Hiyo ni kweli. Ninii tu. . . Maono ni hakika. Kamwe hatujui jinsi yatakavyoendelea ama kile kitakachotukia. Ni juu ya Mungu, na kile-kile kinachotukia. Lakini nilijua, katika kuyangojea, kungojea mambo ya kule.

²⁴⁹ Na hivi majuzi wakati maskini msichana huyu alipokuwa hapa ndani, aliyedhaniwa ana utambuzi, ambao mimi, si. . . Unaona, kama Mungu angaliutoa huo kwa ulimwengu mzima, ingekuwa ni jambo bora sana; lakini kama ingalifanyika hivyo, ingekuwa ni kinyume cha yale Bwana aliyoniambia upande wa pili wa barabara hapa, unaona, miaka michache iliyopita. Nasi tulitaka kuwa na hakika jambo hilo lilikuwa ni kweli, na kuacha kanisa, kwa kuwa jambo hilo lilikuwa liko hapa, walione. Na kwa hiyo kweli nilimwita huyo Bibi Snyder. Dada Snyder. Yuko hapa mahali fulani. Yeye kwa kweli kidogo anapata shida ya kusikia. Na maskini bibi huyo alilizungumza kwa sauti ya chini, na kusema, “Una baridi yabisi,” ama yabisi kavu, kitu kama hicho.

²⁵⁰ Ambapo, mimi nilijua ilikuwa ni nyonga iliyovunjika. Na kwa hiyo. . . Ndipo Roho Mtakatifu alipoleta jambo hilo asubuhi ya leo. Unaona?

²⁵¹ Sasa, jambo ni kwamba, ni karama ya Kiungu, na inafanya kazi katika mamlaka yake. Lakini kile kinacholifanya jambo hilo kuwa gumu sana hapa mjini, kwa kweli, ni—ninakuwa na utata, wakati wote, katika kuwaombea wagonjwa hapa. Ama—ama. . . Nitaenda, niwaambie watu jambo hili. Nitaenda, niseme, “Sasa Bwana amekuponya. Yesu alikuponya wakati alipokufa kwa ajili yako, miaka elfu moja mia tisa iliyopita. Uliponywa pale pale. Sasa, kulingana na Mungu, kulingana na Kristo, uliponywa, miaka elfu moja mia tisa iliyopita. Ugonjwa wako uliondoka. Inahitaji imani yako kufanya jambo hilo.”

²⁵² Na halafu mtu huyo anaweza akaondoka wala asipone. Halafu mtu huyo anakuja, anasema, “Ndugu Branham aliniambia nilikuwa mzima.” Unaona? Ninawaambieni yale Mungu aliyosema.

²⁵³ Sasa, wakati linaponenwa moja kwa moja kwa mtu huyo, moja kwa moja, “Ni BWANA ASEMA HIVI,” juu ya jambo fulani litakalotukia. Hilo litakuthibitishia papo hapo ya kwamba uponyaji wako tayari umepatikana. Imani yako imetia muhuri jambo hilo. Unaona? Ahadi hiyo ni yako. Si neno langu. Ni Neno la Mungu, ya kwamba umeponywa tayari. Unaona? Lakini unaninii tu. . . Kwa njia moja ama nyingine, mimi si—siwezi tu kulifanya lizame ndani, kwa jamaa wa hapa Jeffersonville. Si—siwezi tu kulifanya litukie. Ninajua. Nitajaribu kuelezea jambo hilo vizuri tu niwezavyo, na halitaninii tu—halitatendeka tu. Hivyo tu. Ninasema. . .

254 Hapa, si muda mrefu uliopita, nilienda kwenye nyumba moja, kwa mtu fulani, naye mtu huyo alikuwa anakufa. Nao wakaniita, “Njoo, umwombee. Daktari alisema asingeishi mpaka ifikapo asubuhi.”

255 Nikaingia. Ndipo kijana mwamamume huyo akaniambia, “Bw. Branham, sitaki kufa.” Mbona, bila shaka maskini kijana mwanamume huyo hakutaka kufa. Alikuwa na familia ya watoto wawili pale.

256 Vema, nikaketi. Nikasema, “Sasa, angalia, daktari wako ni nani?” Akaniambia. Nikasema, “Sasa, huenda daktari alisema ulikuwa unakufa, utakufa, bali Mungu bado hajasema ulikuwa unakufa.” Nikasema, “Sasa, kulingana na Biblia, umeponywa tayari, kwa kuwa Yesu alikufa kwa ajili ya uponyaji wako.”

257 Akasema, “Je! unaamini nitakuwa mzima?”

258 Nikasema, “Kabisa ninaamini hivyo.”

259 Vema, kama nilienda kumwombea mtu, wala sikutumia imani ya namna hiyo, kuamini kwa ajili yake; kama nikienda, “Loo, la, la, kama daktari alisema utakufa, utakufa. Sasa hilo linayakinisha jambo hilo.” Sasa, je! huyo asingekuwa ni mtu kweli wa kuja kumwombea mgonjwa? Nisingemtaka mtu huyo nyumbani mwangu, kuniombea. Ninataka mtu fulani ambaye, hata kama hakuliona hilo, au la, angechukua imani na kusimama kwenye ahadi kwa ajili yangu. Hiyo ni kweli. Nami nilisema . . . yeye . . .

260 Tulienda na tukaomba. Nikasema, “Sasa uwe hodari.”

261 Akasema, “Unataka kusema nitakuwa mzima?”

262 Nikasema, “Mbona, hakika. Neno la Mungu lilisema utapona. Unaona, ‘Kama unaweza kuamini, mambo yote yanawezekana.’”

263 Akasema, “vema, nitaamini Hilo.” Ndipo akatoka akaenda akamwambia mke wake, hilo.

264 “Mtu huyo anakufa, sivyo?”

265 “Naam, anakufa.” Na kwa hiyo kesho yake, mtu huyo akafa, ama siku chache baadaye.

266 Ndipo mwanamke huyu anatoka na anaanza kunywa na kufanya yasiyofaa. Ndipo mmoja wa mashemasi, ninaamini ilikuwa ni mmoja wa hao mashemasi, wa kanisa hili, alimwendea mwanamke huyo na kumsihi kama angeweza kurudi na kuja kanisani. Akasema, “Nisingeweza kumwamini mtu yeyote. Mhubiri Branham aliingia hapa na akamwombea mume wangu, akasema ataishi, naye akafa siku mbili ama tatu baadaye.” Kasema, “Nisingeamini.” Sasa *huyo* mama anakufa. Vema.

267 Lakini, hata hivyo, unaona, inaonyesha ya kwamba watu hawasilizi yale unayosema. Unaona? Hakika. Kama nilimwombea mtu fulani, nami ni—niwaambie watu hao

wataishi. Ninaamini wataishi. Lakini, haidhuru, kama neno langu lilikuwa ni BWANA ASEMA HIVI kabisa, nawe usiliamini, ungekufa, hata hivyo. Hakika. Hili *hapa* BWANA ASEMA HIVI, na wengi wao wanalipokea na wanakufa. Wengi wao wanaenda kuzimu, wakati ni, BWANA ASEMA HIVI, “Si lazima mwende.” Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Hakika. Mnaona? Ni kile. . . Yote yana msingi wake katika imani yako.

²⁶⁸ Ndugu Collins, sidhani yuko hapa usiku wa leo. Lakini nilipokuwa nikimsikiliza asubuhi ya leo, alihubiri vizuri sana juu ya jambo hilo. Unaona? Unaona? Alihubiri. Alisema, “Sasa, imani ile ile uliyo nayo hapa, itakubidi uwe nayo huko. Kwa sababu, ni imani yako binafsi, si imani katika madhehebu yako, bali katika Kristo. Huna budi kuwa na imani hiyo.” Hiyo ni kweli kabisa. Kabisa.

²⁶⁹ Na uponyaji wa Kiungu umewekwa msingi wake juu ya imani yako. Lakini kulingana na Neno la Mungu, BWANA ASEMA HIVI, ni kwamba kila mtu aliponywa wakati Yesu alipokufa pale Kalvari, “Alijeruhiwa kwa makosa yetu, kwa mapigo Yake sisi *tuliponywa*.” Hiyo ni kweli? *Tuliponywa*. Biblia ilisema, “Mliponywa.” Kwa hiyo usitafute makosa kwangu, mimi ni mhubiri tu wa Neno. Nenda ukamwambie Mungu ya kwamba Yeye alisema jambo la uongo, naye Mungu atakwambia mahali udhaifu wako ulipo basi. Unaona? Kwa hiyo, ni imani yako. Yesu alisema, “Kama unaweza kuamini.” Kama unaweza kuamini.”

²⁷⁰ Sasa, unaposikia Roho Mtakatifu amethibitisha imani yako na kuiimarisha, na kusema, “BWANA ASEMA HIVI, ‘Kesho wakati *kama* huu, utapata kitu *fulani*. Kitu *fulani* kitatukia. Kitakuwa hapa kwa njia *fulani*, nawe utakuta kitu *fulani* hapa. Hiyo itakuwa ni ishara kwako.’” Sasa, wewe angalia jambo hilo. Hiyo ni kazi iliyomalizika, papa hapa sasa.

²⁷¹ Lakini wakati inafikia kuzungumzia uponyaji wa Kiungu, sina budi kuweka uponyaji wa Kiungu kwenye msingi ule ule, wa namna hiyo, kama wokovu. Kila mmoja wenu, haidhuru mmefanya nini, mmeokolewa tangu Yesu alipokufa, maana Yeye alikufa apate kuondoa dhambi za ulimwengu. Bali kamwe halitakusaidia hata kidogo mpaka wewe mwenyewe ulikubali na litukie kwako. Lakini kuhusu dhambi zako, tayari zimesamehewa. Hiyo ni kweli. Yeye. . . “Tazama Mwana-Kondoo wa Mungu azichukuaye dhambi za ulimwengu.” Unaona? Hilo hapo. Sasa kumbukeni jambo hilo.

²⁷² Sasa, ninajua ya kwamba katika kufundisha, katika Maandiko, sisi ni kusanyiko lililochanganyikana. Na mara nyingi, katika Kitabu hiki cha Waebrania, ambacho kwa namna fulani ni Kitabu chenye kilindi. . . Itanibidi kukiacha kwa muda kidogo sasa. Nitajaribu usiku wa leo kumaliza sehemu ya mwisho ya mlango huo wa 7.

²⁷³ Na sasa kuna maswali mengi kwenye mawazo yenu, hapana shaka. Wengi wenu mna maswali, na mimi ninge kuwa nayo, pia. Sasa, wakati mwingine, Bwana akipenda, nitakaporudi . . .

²⁷⁴ Ninaenda Michigan sasa. Na halafu, kutoka Michigan, ninaenda Colorado. Na kutoka Colorado, mpaka Pwani ya Magharibi. Sasa—sasa, tutakaporudi, Bwana akipenda . . . Sasa, sijui. Kama sitakuwa Chicago, Jumapili, huenda nikarudi hapa kwa ajili ya Jumapili ijayo jioni.

²⁷⁵ Sasa tunamtoa mchungaji wetu kwenye mimbara hapa kwa majuma kama sita, katika ninii zote hizi—hizi—hizi, kitabu hiki hapa. Unaona? Sasa sisi . . . Mimi sipendi kufanya jambo hilo. Ndugu Neville ni ndugu mzuri, mwema, na mpole. Nami nina hakika ya kwamba kanisa hili linampenda Ndugu Neville.

²⁷⁶ Licha ya hayo, wakati nikizungumza; mtu fulani, mahali fulani humu nchini, ana hatia ya kuandika vijitabu, kumwondosha Ndugu Neville mimbarani. Itakubidi kutatua jambo hilo na mimi. Aa. Hiyo ni kweli. Aa. Naam, kweli. Sasa, ninawatakeni . . . Kasema shema- . . . kitu fulani kuhusu halmashauri ya mashemasi. Halmashauri ya mashemasi haina mamlaka yoyote juu ya mchungaji huyo. La, bwana. Kusanyiko, zima, lina mamlaka yote. Si ninii . . . Halmashauri ya mashemasi ni polisi tu hapa kanisani, ni kudumisha tu utaratibu na kadhalika. Lakini inapokuja kwenye swala la kanuni, kanisa lote ndilo lenye mamlaka. Kanisa hili limejengwa juu ya mamlaka ya kujitawala lenyewe hapo mahali lilipo. Kwa hiyo, mimi sina jambo la kusema juu ya kuondolewa kwa mchungaji huyu, ama kumweka mwingine. Mimi ninamiliki rasilimali hii; imetolewa kwa kanisa. Ninyi nyote ndio hilo kanisa. Ninyi watu ndio mlio na amri juu yake. Ninyi ndio kanisa, ninyi wenyewe. Nalo Kanisa, Kanisa takatifu la Mungu ndilo utawala, wa Roho Mtakatifu katika Kanisa hilo. Na mimi jambo pekee ninalofanya ni kumiliki rasilimali, na kulipa rasilimali hiyo kanisa hili, kama kuitoa tu kwa ajili ya kanisa, nayo hailipwi kodi. Nalo kanisa huchagua wachungaji wao wenyewe, mimi sihusiki chochote na jambo hilo. Na namna pekee mchungaji huyu angaliweza kuondoka, ni mchungaji aamue mwenyewe kuondoka, ama wingi wa kura za kanisa itabidi useme, “Mbadilisheni mchungaji.” Hiyo ndiyo njia pekee. Hakuna halmashauri ya mashemasi inayoweza kufanya hivyo. Halmashauri ya mashemasi huweka tu utaratibu na kadhalika kanisani.

²⁷⁷ Wadhamini, hawana mamlaka yoyote na jambo hilo, ni kurabati tu kanisa. Wala hawawezi kulirekebisha mpaka pasiwepo na . . . Halmashauri yote ya wadhamini inakutanika na kusema, “Tutajenga *hili*, ama tutafanya *lile*.” Ndipo inawabidi kumwuliza mweka hazina kama wana fedha za kufanya jambo hilo. Naam, bwana.

²⁷⁸ Lakini kukiwa na shtaka lolote dhidi ya mfuasi yeyote, kama mfuasi ananung'unika dhidi ya mwingine, ama kuna kasoro fulani, unapaswa kumwendea ndugu huyo, wewe mwenyewe; na kuzungumza naye, wewe na yeye peke yenu. Ndipo kama hawatalipokea, basi jambo linalofuata, unamchukua mmoja wa mashemasi ama mtu fulani, kisha mwende pamoja naye kwa ndugu huyo. Ndipo asipolisikiliza, basi njoo uliambie kanisa. Ndipo endapo kanisa . . . Ndipo asipolikubali kanisa, basi Biblia ilisema, "Acha wawe kama mtu wa mataifa na mtoza ushuru." Hiyo ni kweli.

²⁷⁹ Na mtu ye yote anayejua mtu mwenye hatia, wala huwaendei na kuzungumza, basi wewe ni sehemu ya kanisa la Mungu itakayojibu kwa dhambi hiyo. Hiyo ni kweli.

²⁸⁰ Na endapo basi watu wowote wana—wana nung'uniko dhidi ya shemasi, ama dhidi ya shemasi ama mtu fulani kanisani, inatakiwa watu watatu. Watu watatu wangekuja na kusema, washuhudie, kinywa cha mashahidi wawili ama watatu. Waje wamwambie mchungaji ya kwamba kuna shtaka dhidi ya shemasi. Ndipo kama kuna shtaka dhidi ya shemasi, shemasi si mtu mwenye—mwenye haki, mtu m—mwaminifu. Anapaswa kushikilia kazi ya shemasi, bila lawama, na kisha asipatikane na lawama. Na kama kusanyiko hilo likikuta kwamba shemasi huyo hasimamii ofisi hiyo, anawachukua watatu pamoja naye na kulipeleka kwa mchungaji. Shemasi huyo anaombwa kukaa nyumbani usiku huo. Ndipo basi mchungaji kutoka . . . anakuja na kulikusanya kusanyiko pamoja, anatoa hilo lalamiko. Na kama kusanyiko likipiga kura kwamba shemasi huyo aendelee, huyo shemasi anaendelea. Kama akininii . . . wakipiga kura shemasi huyo aondolewe, wanamchagua shemasi mwingine usiku uo huo. Mnaona?

²⁸¹ Kwa hiyo, hakuna mtu mmoja peke yake anayehusika na lolote la kuamua katika jambo hili. Ni wingi wa watu. Naam, bwana. Kama ishirini wakimpigia kura, na ishirini na mmoja wapige dhidi yake, anaondoka; ama, na vinginevyo vivyo hivyo. Unaona? Hayo ni, ni mamlaka makuu kabisa ya kanisa la mahali hapo na, basi, kila mmoja wa washiriki hao ana jambo la kusema kanisani. Chochote kikienda, vibaya, ndipo wanaweza kuja moja kwa moja hapa, na jambo pekee wanalopaswa kufanya ni kukaa mbele za Mungu na kuona kabisa ya kwamba hakuna kinachozuia mwendeleo wa kanisa.

²⁸² Lakini mamlaka yote na kamili ya kanisa ni mchungaji. Soma hayo katika Biblia, angalia kama hayo si utaratibu ulioko katika Biblia. Hiyo ni kweli kabisa. Hakuna mtu aliye juu ya mzee wa kanisa. Sihusiki na lolote lile Ndugu Neville analofanya hapa. Hiyo ni juu yenu na Ndugu Neville. Kama Ndugu Neville alitaka kuhubiri fundisho la Mashahidi wa Yehova, hilo ni juu yake na juu yenu. Unaona? Kama alitaka kuhubiri chochote alichotaka, hilo ni kati yenu na yeye. Hivyo tu. Kama kusanyiko

hilo likimpigia kura, kuhubiri hilo, hilo ni sawa. Hilo ni juu yake.

283 Jambo pekee ninalofanya, ni kumiliki rasilimali hii tu. Na kama jambo moja ama lingine likitukia, ambalo ni kama kumwondosha mchungaji, nao wanataka kupigia hilo kura, msingemwuliza shemasi kufanya jambo hilo. Mngenijia mimi. Ningeshuka nije, niseme, “Kama mnataka kumwondosha mchungaji, niambieni ni kwa nini. Je! amefanya lo lote?”

284 “Ndiyo. Tulimshika, amelewa. Ama, tulimshika akifanya jambo *hili*, ama akifanya jambo ambalo halikuwa zuri.”

285 “Je! mna mashahidi watatu wa jambo hilo?”

286 “Naam. Tunao.”

287 Hao mashahidi hawana budi kujaribiwa kwanza. “Msipokee shtaka lolote dhidi ya mzee ila iwe ni kwa mashahidi wawili ama watatu, na hawana budi kuthibitishwa kwanza; dhidi ya mzee.” Halafu inawabidi kuapa kwa jambo hilo, ya kwamba uliliona; na kulithibitisha, ya kwamba uliliona.

288 Na ndipo basi, kama ulimwona, basi dhambi hiyo inakemewa wazi wazi, ya kwamba, “Ni kosa.” Kisha msemi, “Kusanyiko, je! mnataka kumbadilisha mchungaji wenu?”

289 Na kama kusanyiko likipiga kura, “Msameheni, na acheni aendelee bado,” hivyo ndivyo inavyopaswa kuwa. Unaona? Hiyo, hiyo si ndiyo njia bora kabisa ya kuliendesha kanisa? Hivyo ndivyo Biblia ilivyosema. Hatuna maaskofu wala wasimamizi, na halmashauri na kadhalika, kumwingiza *huyu* na ina mamlaka mengi sana. Hakuna mtu aliyenye na mamlaka hapa ila Roho Mtakatifu. Hilo ni kweli. Yeye ndiye anayeondoa. Nasi tunamchukua kwamba Yeye ni wingi wa watu, jinsi ambavyo watu wanaelekea.

290 Na ndipo kama upande mmoja unataka kufanya jambo *hili*, na upande huo mwingine unataka kufanya jambo *lile*, na upande huo unashinda. Upande ulioshindwa, watafanya nini juu ya jambo hilo? Watajiunga moja kwa moja na hao wengine, waseme, “Tulikosea, basi. Tutaendelea moja kwa moja, maana Roho Mtakatifu amefanya chaguo hilo.” Unaona? Hilo ni sahihi kabisa.

291 Ni kama vile Wademokrasia na Waripablikan, mradi tu tunasimama kama demokrasia, kama Wamarekani. Kama Wademokrasia wametwaa ushindi, Waripablikan wanapaswa kusonga mbele moja kwa moja pamoja nao; Waripablikan wakishinda, Wademokrasia wanasonga mbele Unaona? Hilo ndilo hasa linalotufanya sisi kuwa taifa. Wakati wowote tutakapovunja hilo, tunavunja Demokrasia yetu. Hiyo ni kweli. Wanademokrasia wanasema, “Sitafanya lo lote; Waripablikan ndio walioshinda.” Basi tunaanguka. Mimi ni Mkentakake: umoja ni nguvu, na tukigawanyika tunaanguka.

²⁹² Sasa, kama kuna jambo lo lote baya kanisani unalojua habari zake, jamaa fulani ama mtu fulani ama cho chote kile, mnawajibika na mtawajibika mbele za Mungu kama hamlitatui jambo hilo; ninyi, kanisa. Sasa, kumbukeni, haliko mabegani mwangu. Liko juu ya yenu. Na cho chote kibaya kanisani Mungu atawataka mjibu. Hiyo ni kweli. Hivyo ndivyo Yeye anavyoliendesha kanisa Lake. Hivyo ndivyo ilivyo katika Biblia. Huo ndio utaratibu wa Biblia. Hayo ndiyo mamlaka makuu kabisa ya kanisa la mahali. Mchungaji ndiye kichwa. Hiyo ni kweli. Amina.

²⁹³ Sasa, nikija kwenye Ujumbe huu wa kale uliobarikiwa hapa. Ninyi, sasa nawatakeni mjue jambo hilo. Huu unarekodiwa kwenye kanda, kumbukeni, Ujumbe huu. Na urekodishaji wa kanda wa kanisa, taratibu na kanuni za kanisa, yako yamerekodiwa kwenye kanda. Hiyo ni kulingana na Biblia. Hatuliendeshi sisi; hakuna mtu anayeliongoza. La. Wote, sisi sote ni sawa. Lakini, tuna kiongozi, huyo ni mchungaji, mradi tu anaongozwa na Roho Mtakatifu. Kweli. Vema.

²⁹⁴ Sasa, katika haya, kutakuwa na maswali mengi sana. Kwa hiyo watakaposambaza tena . . . Naye Ndugu Neville akitangaza kwenye redio ya kwamba nitapaswa kuwapo hapa, hebu andika swali lako, ili mimi na wewe tuweze kulibishania. Sivyo? Sawa.

²⁹⁵ Ninajua nimehubiri juu ya uvumilivu wa watakatifu. Nimefundisha juu ya Uungu mkuu wa Yesu. Nimefundisha juu ya usalama wa mwaminio, na kuchaguliwa tangu zamani, kuteuliwa tangu zamani, na mengi ya mambo hayo. Jambo ambalo, ninajua, katika kusanyiko langu kuna washika sheria wengi, kitu ambacho ni sawa kabisa. Kweli kabisa. Lakini, sasa, mambo hayo, mimi pia ni mshika sheria, nami ni Mkalvini. Ninaamini tu Biblia. Hivyo tu.

²⁹⁶ Sasa, kama baadhi ya hayo, maswali. Nami nimefundisha juu ya madhihirisho, mihemuko, na kadhalika, na mambo hayo yote ambayo huenda hamkukubaliana nayo. Kwa hiyo moja ya siku hizi usiku, labda . . . Hebu na tulitatie . . .

Je! mna haraka sana ya kurudi humu ndani? [Ndugu Neville anasema, "La."—Mh.]

Hebu na tulifanye Jumatano usiku, usiku wa Jumatano hii ijayo, ndipo ni—ninafikiri ni—ninaweza kuwa na mambo hayo basi. Lete swali lako Jumatano usiku, liweke hapa jukwaani, na swali kuhusu Biblia, vema, juu ya yale niliyokuwa nikifundisha sasa. Na Jumatano usiku. Kisha kufikia Jumapili ifuatayo, basi, nafikiri sina—sina budi kuwa huko Chicago, hata hivyo. Nami ninaenda kutoka huko kuingia Michigan. Bwana akipenda, nitakuwa hapa Jumatano usiku, kujaribu kujibu swali lako vizuri niwezavyo. Na sasa Bwana na aturehemu.

Sasa hebu na tuinamishe kichwa chetu, dakika moja tu.

297 Sasa, Bwana tunayekuaadhimisha, huu ni mpango Wako mkuu. Ni kanisa lako. Ni Wewe, Bwana, unayetenda kazi, nasi tunataka kusonga mbele jinsi Roho wa Mungu anavyotusogeza. Nasi tunaomba sasa ya kwamba utatubariki. Na tunapourudia Ujumbe huu, na kuingilia mambo haya yenye kilindi, tunaomba ya kwamba Roho Mtakatifu atatufunulia hayo jinsi tu tulivyo na haja nayo. Kwa kuwa tunaomba katika Jina Lake. Amina.

298 Sasa, loo, mimi... Kitabu hiki cha Waebrania, ninakithamini kama kimojawapo cha Vitabu vikuu.

299 Baadaye kidogo, huenda ikawa kwamba ni—nina... ninaenda nchi za ng'ambo, ambapo hilo, Bwana akiliruhusu, nitafanya hivyo hivi karibuni sana. Inanibidi kwenda Afrika kulingana na ono. Nafikiri kamwe sitafanikiwa sana katika mikutano yangu mpaka nitakapoenda Afrika na kutimiza ono hilo. Sasa, basi, hilo litakuwa labda ni wakati mwingine kwenye majira haya yajayo ya kuchipua.

300 Lakini katikati ya wakati huo, nataka kuchukua kitabu kingine kimoja zaidi kutoka katika Kitabu cha Waebrania, hicho ni, mlango wa 11 wa Waebrania. Na kukaa kama juma moja katika mlango huo wa 11, na kuchukua kila moja ya sifa hizo ama hao watu, na kufafanua sifa zao. Unaona? “Kwa imani, Nuhu,” ndipo nichukue maisha ya Nuhu. “Kwa imani, Ibrahimu,” ndipo niyachukue maisha ya Ibrahimu. “Kwa imani, Habili,” ndipo niyachukue maisha ya Habili. Unaona? Na nifafanue hayo. Je! mngependa jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Loo, hilo lingekuwa, tutachukua Biblia nzima basi. Na ndipo tutajaribu jambo hilo, labda, aidha katika, tuseme, juma moja ama siku kumi za mikutano, mkutano mmoja tu baada ya mwingine, katika namna kama ya ufufuo, wakati mwingine kwenye likizo ya Krismasi, ama kitu kama hicho, Bwana akipenda.

301 Sasa, katika mlango wa 7 wa Kitabu cha Waebrania, tulikutana na Mtu huyu mkuu. Ni nani anayeweza kuniambia Jina Lake lilikuwa ni nani? [Kusanyiko linasema, “Melkizedeki.”—Mh.] Melkizedeki. Sasa, huyu Melkizedeki alikuwa ni nani? Alikuwa ni kuhani wa Mungu Aliye Juu Sana. Alikuwa ni Mfalme wa Salemu, ambaye alikuwa ni Mfalme wa Yerusalemu. Hakuwa na baba yeyote, ama hakuwa na mama yeyote. Hakuwa na wakati aliopata kuzaliwa, wala hatakuwa kamwe na wakati atakapokufa. Sasa, tunaona ya kwamba huyo hana budi kuwa ni wa Milele.

302 Tuliona ya kwamba Neno *daima* linamaanisha “kipindi cha wakati.” Je! mngali mnakumbuka jambo hilo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Kipindi cha wakati, ni daima na daima. Na *daima* limeonekana, mara nyingi, katika Biblia kama “ki—kipindi cha wakati.”

³⁰³ Lakini, Umilele, na kuna aina moja tu ya Uzima wa Milele, tuliona. Hiyo ni kweli? Mungu ana huo Uzima wa Milele, pekee Yake. Hiyo ni kweli? Aina moja tu ya Uzima wa Milele. Hakuna neno kama “adhabu ya Milele.” Maana, kama utaadhibiwa Milele, huna budi kuwa na Uzima wa Milele. Kuadhibiwa Milele, ingekubidi kuwa na Uzima wa Milele. Na kama una Uzima wa Milele, huwezi kuadhibiwa, unaona, kama una wa Milele. “Yeye ayasikiaye Maneno Yangu, na kumwamini Yeye aliyenipeleka, yuna Uzima wa milele.” Hiyo ni kweli? Uzima wa Milele, kwa maana unaamini. Vema, kama una Uzima wa Milele, huwezi kuadhibiwa, kwa maana una Uzima wa *Milele*. Kwa hiyo, basi, kama utateseka jehanamu milele na milele, huna budi kuwa na Uzima wa Milele.

³⁰⁴ Lakini, sasa, ninaamini ya kwamba Biblia inafundisha habari za jehanamu halisi inayowaka moto. Biblia inafundisha jambo hilo, ya kwamba dhambi na uovu hayo yataadhibiwa, milele na milele. Hiyo si Umilele, sasa. Hiyo huenda ikawa ni kwa miaka bilioni kumi. Huenda ikawa ni kwa miaka bilioni mia moja, lakini wakati fulani haina budi kukoma. Kwa kuwa, kila kitu kilichokuwa na mwanzo, kina mwisho. Ni vitu vile visivyo na mwanzo, havina mwisho.

³⁰⁵ Mnakumbuka somo hilo sasa? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Jinsi tulivyorudi nyuma na kupata ya kwamba kila kitu kilichokuwa na mwanzo kilikuwa kimepotoshwa, unaona, kupotoshwa kutokana na kitu chenyewe cha kwanza. Na, hatimaye, ni jambo linaloishia katika Umilele. Ndipo basi kuzimu yote, mateso yote, na kumbukumbu lote la hayo, vitatoweka Milele. Kila kitu kinachoanza, hukoma.

³⁰⁶ Naye huyu Melkizedeki hakuwa ni Yesu, kwa kuwa Yeye alikuwa ni Mungu. Na kile kilichowafanya Yesu na Mungu kuwa tofauti, ni kwamba, Yesu alikuwa ni maskani alimoishi Mungu. Unaona? Sasa, Melkizedeki. Yesu alikuwa na baba na mama pia. Naye Mtu huyu hakuwa na baba wala mama kamwe. Yesu alikuwa na mwanzo wa maisha Yake na alikuwa na mwisho wa maisha. Mtu huyu hakuwa na baba, hakuwa na mama, hakuwa na mwanzo wa siku Zake wala mwisho wa uhai Wake. Lakini, ilikuwa ni Mtu yule yule, ilikuwa hivyo. Melkizedeki na Yesu walikuwa ni Mmoja; lakini Yesu alikuwa ni mwili wa duniani, uliozaliwa na kuumbika kwa jinsi ya dhambi. Mwili wa Mungu Mwenyewe, Mwanawe wa pekee, aliyezaliwa na kuumbika kwa jinsi ya dhambi, apate kuung’oa mwiba kutoka katika mauti, apate kulipa deni, na kuwapokea wana na mabinti Kwake. Mnalipata? Hiyo ndiyo sababu ya kwamba Yeye alikuwa—alikuwa na mwanzo, Yeye alikuwa na mwisho.

³⁰⁷ Lakini mwili huu mkamilifu, katika kumbukumbu, kama—kama ishara ya kufufuka kwetu, Mungu asingeruhusu mwili huo mtakatifu uone uharibifu, kwa maana Yeye Mwenyewe ndiye

aliyeumba. Na akauleta uzaliwe, na akaufufua, na kuuweka mkono Wake wa kuume.

³⁰⁸ Na, leo, Roho Mtakatifu aliyeufufua mwili huo yuko hapa Kanisani. Jina la Bwana litukuzwe! Na akionyesha miujiza ile ile na nguvu. Na siku moja huyu Roho Mtakatifu, aliye Kanisani, atanguruma na atainuka juu, naye atajipokea mwenyewe katika umbo la mwili huu unaoketi katika mkono wa kuume wa ukuu wa Mungu, ili kufanya upatanisho kwa ajili yetu sisi wenye dhambi. Na sisi Hapo tunawekwa mbali na dhambi kikamilifu. Si kwamba hatutendi dhambi; bali tumewekwa mbali na dhambi, Mbele za Mungu. Maana, kuna dhabihu ya Damu inayosimama kati yangu na Mungu, kati yako na Mungu. Hiyo ndiyo sababu Yeye alisema, “Mtu aliyezaliwa na Mungu, hatendi dhambi, hawezi kutenda dhambi.” Kwa kuwa, kama umezaliwa mara ya pili, Roho Mtakatifu yeye yule aliyeishi katika ule Mwili anaishi ndani yako. Na hauwezi kutenda dhambi; dhabihu imewekwa mbele Zake. Ndipo kama ukitenda dhambi makusudi, inaonyesha ya kwamba haiwezekani kwako kuwa katika Mwili huo. Amina. Hiyo ndiyo Injili. Hiyo hapo.

³⁰⁹ Kwa hiyo, unaona, haipingi Maandiko yo yote. Inayaunganisha Maandiko pamoja. Unaona? “Isingewezekana kwa hao waliokwisha kupewa nuru.” Hapo ndipo tutakapopata maswali yangu. Kwa kuwa, yaleteni tu, hivyo ndivyo tunavyotaka.

³¹⁰ Sasa angalia. “Haiwezekani kwa hao waliokwisha kupewa nuru, kuanguka wapate kujifanya upya tena hata wakatubu, kuona kwamba wanamsulibisha Mwana wa Mungu upya, na kumfanya...na kumdhihaki kwa dhahiri.” Wasingeweza kufanya hivyo.

³¹¹ Ndipo unaenda kwenye Waebrania 10, ambapo linasema pale, “Kwa kuwa kama tukitenda dhambi makusudi baada ya kupokea ujuzi wa ile Kweli.” Na dhambi ni kitu gani? Kutokuamini.

³¹² Kama kwa makusudi ukimwona Roho Mtakatifu akifanya mambo ambayo Yeye alifanya papa hapa asubuhi ya leo, na uone ya kwamba Kristo amefufuka kutoka katika wafu, Naye anaishi katika Kanisa Lake na miongoni mwa watu Wake, nawe unalighairi makusudi, haiwezekani kwako kumjia Mungu kamwe, maana umemkufuru Roho Mtakatifu.

³¹³ Yesu alisema mambo yayo hayo, wakati alipokuwa akifanya miujiza hiyo.

³¹⁴ Wao walisema, “Mbona, Yeye ni Beelzebuli. Yeye ni mpiga ramli. Yeye ni ibilisi.”

³¹⁵ Yesu aligeuka, na kusema, “Nitawasamehe kwa ajili ya jambo hilo. Lakini wakati Roho Mtakatifu atakapokuja na mtu ufanye jambo hilo, kunena neno moja dhidi Yake hakutasamehewa kamwe katika ulimwengu huu ama

ulimwengu ule ujao. Kwa kuwa umemwita Roho wa Mungu aliyekuwa ndani Yake, 'Pepo mchafu.'"

³¹⁶ Basi, kama tukifanya dhambi makusudi, kama tukifanya dhambi, tusiamini makusudi. Si baada ya kuipokea ile Kweli, tumezaliwa mara ya pili; tusingeweza kufanya dhambi baada ya kuzaliwa. Mwenye dhambi hawezi kufanya dhambi isiyosamehe-... Mkristo hawezi kufanya dhambi isiyosameheka. Hawezi kufanya jambo hilo. Walio waovu ndio wanaofanya hivyo. Ni anayejifanya mwaminio, sio mwaminio.

³¹⁷ Wale marabi wa Kiyahudi, loo, walidhani walikuwa watu wa hali ya juu, nao walikuwa na Ma-D.D na Ma-Ph.D. Walidhani wanajua kila kitu, bali walikuwa wenye dhambi walio waovu sana. Loo, huenda... Usingeweza kuwanyooshea mkono, juu ya maisha yao. Walikuwa ni wasafi, waadilifu, na wenye haki, kwa jinsi hiyo. Bali walikuwa ni Wasioamini.

³¹⁸ Na hebu uchukue neno dhambi na uone maana yake. Neno *dhambi* linamaanisha "kutokuamini." Kuna makundi mawili tu, hayo ni, mwaminio ama asiye mwaminio. Yaani, mtu aliyehesabiwa haki ama mwenye dhambi. Hayo tu. Kama wewe ni asiyeamini, wewe ni mwenye dhambi; haidhuru wewe u mwadilifu kiasi gani, jinsi gani unavyoenda kanisani, ama hata kama wewe ni mhubiri. Ungali ni asiyeamini.

³¹⁹ Wale Mafarisayo walikuwa ni wahubiri, nao walikuwa ni wasioamini, nao wako kuzimu leo kwa ajili ya jambo hilo. Washika dini kabisa walivyoweza kuwa, na wacha Mungu, bali hawakumwamini Yeye. Nao walimwita "pepo," na wakakanusha Neno Lake. Na baadhi yao walisema, "Kama ukiwa wewe ni ninii, sasa shuka msalabani. Fanya muujiza. Hebu tukuone ukifanya hilo." Mmoja alimpiga kichwani, kwa fimbo, na kusema, "Tabiri na utwambie ni nani aliyekupiga, wewe nabii, nasi tutakuamini." Unaona, wasioamini! Wanajifanya kuamini ya kwamba wao walikuwa ni waaminio, bali walikuwa ni wasioamini, wasioongoka, wametengwa, ingawa walikuwa ni watakatifu na ni wacha Mungu.

³²⁰ Hata sasa, jambo lilo hilo ndilo linalosimama siku hizi. Wanaume na wanawake wanaweza kwenda kanisani na wamekunja uso, na—na ni wacha Mungu wawezavyo kuwa, na hawasemi uongo hata siku moja, hawaibi, na wanajitahidi kuiishi dini yao vizuri wawezavyo. Lakini, isipokuwa wawe ni waaminio, wamepotea. Kwa hiyo hakuna dalili ya washika sheria katika Biblia. Ukalvini ni... Neema ni vile Mungu alivyokutendea, na matendo ndiyo unayomfanyia Mungu. Vimetenganishwa kabisa.

³²¹ Kama ukiacha kusema uongo, ukiacha kuvuta sigara, ukiacha kuiba, ukiacha kufanya uzinzi, ukiacha yote, uwe umefanya kila kitu, umezishika amri, na ulienda kanisani, ukabatizwa kila Jumapili, ukashiriki Meza ya Bwana,

ukawatawadha miguu watakatifu, ukafanya kila kitu, ukawaponya wagonjwa, na ukafanya mambo haya mengine yote, isipokuwa umezaliwa kwa Roho wa Mungu, ukateuliwa, umepotea. “Si katika uwezo wa yeye atakaye wala yeye apigaye mbio, bali ni Mungu arehemuye.”

³²² Esau alijaribu alivyoweza kuwa Mkristo, wala hakuweza kufanya jambo hilo. Biblia ilisema alilia kwa uchungu sana, akitafuta mahali pa kutubia, wala asingepapata. Kabla hata hajazaliwa, Mungu alimkataa, maana Yeye alijua alikuwa ni laghai mbaya sana moyoni mwake. Mungu kwa kutangulia kujua alijua jambo hilo. Alisema, “Ninampenda Yakobo, na ninamchukia Esau.” Naye Esau alionekana kama ndiye muungwana. Alikaa nyumbani, akimtunza baba yake mzee kipofu, akawalisha ng’ombe, na kila kitu, alikuwa mvulana mzuri.

³²³ Naye Yakobo alikuwa ni kipenzi cha mama, maskini dondoadume mwongo hodari. Hivyo ndivyo alivyokuwa. Huna budi kukubali jambo hilo. Biblia inalikubali, inalisimulia. Alizurura, akifanya kila kitu. Na—na, mama, akimganda mama. Lakini, hata hivyo, Yakobo, pamoja na mema na mabaya yake yote, na njia zake za kidondoadume, yeye bado angali alikuwa anaihesimu hiyo haki ya mzaliwa wa kwanza. Hilo ndilo jambo muhimu sana.

³²⁴ Esau alikuwa mwungwana maradufu ya Yakobo. Kama ingalikuwa ni swala la sisi kumpima leo, apate kuwa mfuasi wa kanisa letu, ungemchukua Esau, mara elfu moja kwa mara moja, kama usingalimjua. Bali Mungu alimchukua Yakobo.

³²⁵ Ungefanyaje na Mtakatifu Paulo, kama angalitaka kuwa mhudumu? Maskini Myahudi mdogo mwenye pua kama ya ndoana, na mdomo umekaa upande, akienda zake akisumbua tu, na jinsi atakavyoenda kulirarua Kanisa. Anaenda kufanya kila kitu. Ungalifikiri alikuwa amefanya dhambi isiyosameheka. Lakini Mungu alisema, “Yeye ni mtumishi wangu.”

³²⁶ Mungu huwachukua watu na kuwafanya kitu cha tofauti, si watu wanamchukua Mungu na kuwa wa tofauti. Mungu humchukua mtu na kumfanya wa tofauti. Si yale ufanyayo, yale unayotaka, yale unayowazia. Ni yale Mungu anayofanya. Haya basi. Na hivyo ndivyo mambo hayo yalivyo.

³²⁷ Sasa, huyu Melkizedeki mkuu, ni hadhithi ya jinsi gani juu Yake hapa! Tunataka kusoma kidogo, mfano huu. Ilitubidi kuyapitia kwa haraka sana. Tutaanzia hapa nyuma kwenye sehemu fulani ya Maandiko, na tutaanzia kwenye kifungu cha 15.

Tena . . . ni dhahiri sana zaidi, kwamba kuna . . . ikiwa kukitokea kuhani mwingine mithili ya Melkizedeki.

³²⁸ Sasa, Melkizedeki alikuwa ni kuhani. Sivyo? Ndivyo alivyokuwa hapa. Tunaona ya kwamba Mungu, hapo mwanzo,

alikuwa ni chemchemi kubwa ya Roho. Sivyo? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Yeye hakuwa na mahali alipozaliwa. Hakuwa na mahali alipokufa. Hakuwa na mwanzo wa siku Zake. Hakuwa na mwisho wa miaka Yake. Yeye alikuwa ni wa Milele tu kama vile Umilele wenyewe ulivyo wa Milele. Yeye kamwe hakuzaliwa. Hajawahi kamwe kufa.

³²⁹ Na hapo ndani, tunaona ya kwamba, Yeye alikuwa na Roho saba za aina mbali mbali. Hilo ni kweli? Biblia ilisema, katika Ufunuo, ya kwamba, “Zile Roho saba zilizo mbele ya Kiti cha Enzi cha Mungu.” Hilo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Zile Roho saba, za namna mbali mbali. Tunaona, kuna rangi saba. Kuna nyakati saba za kanisa pale. Loo, inaendelea tu. Saba ni kamilifu, na Mungu alikuwa mkamilifu. Na zile Roho saba, na Roho hizo zilikuwa ni kamilifu. Ya kwanza ilikuwa ni rangi nyekundu; upendo mkamilifu, ukombozi. Na jinsi gani, kama tungalikuwa na muda, kuelezea rangi hizo na kuonyesha ya kwamba kila moja ya rangi hizo inawakilisha utakatifu wa Mungu. Amina. Rangi hizo, kuna rangi saba za maumbile ya kawaida. Hizo rangi zinawakilisha utakatifu wa Mungu. Na ninii. . . Rangi hizo zinawakilisha nia na makusudi ya Mungu, tabia ya Mungu. Rangi hizo saba, ziliwakilisha nyakati saba za kanisa, nyota saba, malaika saba. Kote katika Maandiko, wahudumu saba, wajumbe saba, jumbe saba, kila kitu ni katika saba saba. Siku saba. Siku sita, na ya saba ni sabato; kamilifu, kitu kizima. Loo, inapendeza mno, kama tu tungalikuwa na wakati wa kuchimba ndani yake na kuzielezea waziwazi, rangi hizo!

³³⁰ Hebu chukua rangi nyekundu. Tunachukua rangi ya kwanza, ni nyekundu. Nyekundu ni nini? Nyekundu ni ishara moja ya hatari. Nyekundu ni ishara ya ukombozi. Na unapoangalia nyekundu kupitia nyekundu, ni rangi gani? Nyeupe. Hilo ni kweli. Kwa hiyo wakati ile Damu Nyekundu ilipomwagika, kufunika dhambi nyekundu; Mungu, akiangalia kupitia kwenye Damu nyekundu, anapoiangalia dhambi nyekundu, inakuwa nyeupe. Mwaminio hawezi kutenda dhambi. La hashu. Uzao wa Mungu, baraka za Mungu, zinakaa juu yake. Mungu hawezi kuona kitu ila Damu ya Mwanawe. Haidhuru iwe ni nini katika Kanisa Lake, chochote kile, Mungu hakioni, kwa maana Yesu anafanya upatanisho, daima, Kuhani Mkuu. Haiwezekani huo uzao kutenda dhambi, wakati Dhabihu kama hiyo iko pale kwa ajili yake, namna hiyo. Hakika hawezi.

³³¹ Na sasa kama unasema, “Vema, hilo linanipa nafasi nzuri. . .” Basi hiyo inaonyesha wewe huko sawa.

³³² Utathamini jambo Hilo. Utalipenda, kama wewe ni Mkristo halisi, kufikia mahali ambapo dhambi itakusumbua sana mpaka usingeweza kuifanya. “Kwa kuwa Mbegu ya Mungu inadumu ndani yake, wala Yeye hawezi kutenda dhambi.” Biblia ilisema,

“Akiisha kutakaswa na Damu ya Yesu, hana shauku ya dhambi tena.” Kama una shauku, moyo wako hauko sawa na Mungu.

³³³ Sasa, utafanya makosa, bali huyafanyi kwa kudhamiria. Unaona? Una—unanaswa kwenye mtego, na kitu chochote unachonaswa, nacho ama kufanya jambo fulani ambalo humaanishi kufanya, bado si dhambi, utatubu mara utakapoona umekosea. Utageuka upesi na kusema, “Sikumaanisha... sikuona jambo hilo.” Utasema hivyo, maishani mwote. Mtu hataki kuwa hivyo, hiyo ndiyo sababu sisi tumepumbaa sana na tumo gizani sana, hapa duniani, ndiyo sababu kuna upatanisho wa Damu kwa ajili yetu, daima, kutufunika wakati wote. Maana, kosa la kwanza tulilokabilia nalo...

³³⁴ Sasa, hilo ndilo wazo lako la kisheria. “Loo, unajua nini? Yule mwanamke alikuwa ametakaswa. Lakini, Mungu atukuzwe, alifanya makosa. Ninajua amerudi nyuma.” Hilo ni kosa. Hajarudi nyuma. Alifanya kosa. Kama alilifanya makusudi, basi yeye hakuwa sahihi, tangu mwanzo.

³³⁵ Kama hakumaanisha kufanya jambo hilo, naye aende mbele ya Kanisa takatifu la Mungu na kulitubia, na kusema, “Nimekosa, tena nisameheni,” mnawajibika kumsamehe. Usipofanya hivyo kwa moyo wako, basi ulipaswa kwenda madhabahuni wewe mwenyewe. Kweli. Huo ndio utakatifu halisi kanisani. Huo ndio utakatifu wa kweli, utakatifu usio wako, bali wa Kristo.

³³⁶ Sina utakatifu wa kumwonyesha. Bali ninategemea Wake, loo, neema Yake, nami ninayo moyoni mwangu. Sikuistahili, hakuna jambo ningaliweza kufanya kuistahili, bali kwa neema aliniita na kunialika nije. Nami nilimtumainia, Naye aliondoa tamaa hiyo kwangu. Ninafanya maelfu ya makosa kila mwezi, kila mwaka. Hakika. Ninayafanya. Lakini ninapoona nimekosea, ninasema, “Mungu, sikumaanisha kufanya jambo hilo, Wewe unaujua moyo wangu. Sikumaanisha kufanya jambo hilo. Nilinaswa kwenye jambo hilo. Sikumaanisha kufanya jambo hilo. Nisamehe, Bwana.”

³³⁷ Kama nimemkosea ndugu yangu, ninasema, “Ndugu, nisamehe. Sikumaanisha kufanya hivyo.” Hakika, Mungu anaujua moyo wangu.

³³⁸ Loo, hivyo ndivyo ilivyo. Hiyo hapo dhabihu ya Damu. Hizo hapo nguvu za Injili, hilo kanisa takatifu likisonga mbele. Si kwa ajili ya jambo ambalo umefanya; ni jambo ambalo hukuwa na uhusiano wo wote nalo. Huo hapo Upatanisho.

³³⁹ Sasa, Melkizedeki huyu, wakati alipojitokeza.

³⁴⁰ Ninataka kuwaambia jambo lingine. Je, ulipata kuchukua kipande cha kioo chenye pembe tatu? Ukichukua kipande cha kioo ambacho kina pembe tatu, na ukiweke hivi kwamba jua liweze kukipiga, kitatoa rangi saba kamilifu. Kipande cha kioo chenye ncha tatu kitatoa upinde wa mvua. Hiyo ni kweli

kabisa. Sasa, kama tungalikuwa na wakati, tungeingilia jambo hilo. Tatu huleta ukamilifu: Baba, Mwana, Roho Mtakatifu; kuhesabiwa haki, kutakaswa, ubatizo wa Roho Mtakatifu. Haya basi. Ukamilifu huja kupitia kwa hao watatu. Mungu akiwa juu ya mwanadamu; Mungu, katika Mtu aliyeitwa Yesu; Mungu, katika Kanisa. Halafu, ukamilifu.

³⁴¹ Mwanadamu alitenda dhambi, ilimradi tu Mungu alikuwa *hapa* juu katika Nguzo ya Moto, Mungu. Mwanadamu alitenda dhambi, hasa, mbele Za Mungu, ilimradi tu Mungu alikuwa katika Nguzo ya Moto, kwa maana alikuwa angali ni kiumbe kichafu, damu ya mnyama iliwekwa mbele Zake.

³⁴² Ndipo Mwana-Kondoo wa Mungu akaja, hatua ya pili dhahiri ya Mungu; Mungu yeye yule, huduma nyingine. Na halafu Mungu huyu katika... alikuwa katika Kristo, alikuwa ni Mungu yeye yule aliyekuwa katika Nguzo ya Moto. Na Mungu yeye yule alifanyika mwili na akakaa kwetu. Na ndipo mwanadamu akamdhihaki, alikuwa angali anawajibika kwa hilo. Hapakuwa na Damu iliyokuwa imemwagwa bado. Hiyo ni kweli. Yesu alisema, “Nitawasamehe.”

³⁴³ Lakini basi Yeye yule aliyefanyika mwili, alifanyika Nguzo ya Moto tena. “Nilitoka kwa Mungu. Ninaenda kwa Mungu.” Hapa tunamwona Paulo akikutana Naye, akienda zake Dameski, Nguzo ile ile ya Moto. Tunamwona Petro akikutana Naye gerezani, Nguzo ile ile ya Moto. Hakika. Nasi tunamwona leo, miongoni mwetu, Nguzo ile ile ya Moto.

³⁴⁴ Bali utimilifu umefikia mahali pale, hivi kwamba mtu wa wastani... Sasa, kama ikitokea kuwapo na Myahudi hapa, ama mtu fulani anayefahamu Agano la Kale. Kulithibitisha, hebu niwaonyeshe. Sina Agano la Kale, sasa hivi. Hili ni—hili ni Agano Jipya. Lakini katika kule kutolewa sadaka kwa ule mkate wa wonyesho uliokuwa umewekwa kwenye sahani ya ule mkate mwembamba, katika dhabihu ya Kiyahudi kwenye kule kusafishwa kwa zile maskani; mwulize Myahudi yeyote; kuhusu vipande hivyo vitatu vya mkate, kipande cha katikati kilivunjwa. Hicho kilikuwa ni Kristo. Kipande cha katikati kilivunjwa; Kristo, mpatanishi. Ilionyesha ya kwamba ilibidi kuwe na kuvunjwa, mahali fulani, kwa ajili ya ukombozi. Na kipande hicho kilihesabiwa ukombozi, kwenye mkate wa kosha.

³⁴⁵ Naye ndiye huyu hapa. Na usiku wa leo, tunapokula ushirika, tunavunja mkate wa kosha, kwa kuwa ni mwili wa Kristo. Naye alivunjwa pale Kalvari, apate kuwa kipatanisho kwa ajili ya dhambi zetu, ili kwamba kupitia katika haki Yake tupate kuwa haki Yake. Kwa sababu, Yeye alifanyika dhambi yetu, kusudi tupate kuwa haki Yake. Ndugu, hiyo ni neema tupu. Kweli kabisa. Hakuna njia, njia nyingine yoyote ungaliweza kulihesabia haki.

³⁴⁶ Sasa, huyu Melkizedeki, Mtu huyu mkuu aliyekutwa njiani. Yeye alitoa, Ibrahimu alimtolea fungu la kumi. Jinsi ambavyo alikuwa ni Mtu mkuu! Sasa angalia, upesi.

Asiye kuwa kuhani kwa sheria ya amri...za jinsi ya mwili...

³⁴⁷ Sasa unaona hiyo amri ya kisheria? Torati ilisema, “Usiue. Usizini. Usiibe.”

³⁴⁸ Yesu aligeuka moja kwa moja, akasema, “Imenenwa kwa watu wa kale, ‘Usiue,’ bali mimi nasema yeye amwoneaye hasira ndugu yake, bila sababu, ameuu tayari. Imenenwa kwa hao, watu wa kale, “Usizini,” bali nawaambia, kila amtazamaye mwanamke kwa kumtamani, amekwisha kuzini naye moyoni mwake.” Haya basi. Hilo linapaswa kuwafundisha wanawake jinsi ya kuvaa, jinsi ya kufanya yaliyo maadilifu. Ukivaa vibaya, na kuwafanya wanaume wakuangalie kwa njia mbaya, una hatia ya kufanya uzinzi, kama sawasawa tu na vile ulifanya tendo hilo. Yesu alisema hivyo.

³⁴⁹ Na ninyi watu mlio na hasira hizi kali za kumwaga damu, ambao daima mnamfokea mtu fulani, hamwezi kuvumilia, na mambo kama hayo. Iweni waangalifu. Una hatia kama ukisema neno (dhidi ya ndugu yako) ambalo si sahihi, lisilo jema, ukizunguka na kumharibia jina. Si lazima umchome mtu kisu mgongoni upate kumwua. Unaweza kumharibia jina na kumwua, kuua ushawishi wake. Ukimsengenya mchungaji wako hapa, useme jambo fulani baya kumhusu yeye, afadhali hata ungalimpiga risasi. Kama ulisema kitu ambacho hakikuwa ni cha kweli juu yake, vema, kitaharibu ushawishi wake kwa watu na vitu kama hivyo, nawe una hatia ya jambo hilo. Ndivyo Yesu alivyosema.

³⁵⁰ Sasa, sikilizeni hapa, yale—yale Paulo aliyokuwa akijaribu kusema hapa. Ninaipenda Biblia hii ya kale. Inakunyosha. Angalia, loo, hebu angalia tu hapa. Sasa, tunaposoma ninii cha...nne.” Ni...kwa kuwa ni dhahiri ya kwamba Bwana wetu alitoka katika Yu-...” Ngoja, ninaamini nina kifungu kingine hapa nilichokuwa naenda kusoma. La, hapa chini katika cha kumi na sita.

Asiyekuwa kuhani kwa sheria ya amri...za jinsi ya mwili...

³⁵¹ Hiyo ni ya kisheria, unaona. “Loo, ndugu, si—sipaswi. Sipaswi. Ninajua, lakini mimi...” Hilo silo. Upendo ndio unaofanya jambo hilo.

³⁵² Jinsi tulivyopitia kwenye jambo hilo! Nilisema, “Kama nilimwambia nanii wangu...khusus mke wangu, ‘Loo, vema, ni—ni—ningetaka kuwa na wake wawili. Ningetaka kuzurura na huyu, nimfanyie hivi pale. Lakini, nikifanya hivyo, mke wangu atanitaliki...Na watoto wangu watakuwa katika...Huduma

yangu ingekufa.” Ewe mnaiki mchafu, uliyeoza. Hiyo ni kweli. Kwanza, humpendi ipasavyo. Hiyo ni kweli kabisa.

353 Kama ungalimpenda, hakutakuwa na sheria juu yake. Ungempenda, hata hivyo, nawe ungeshikamana naye. Hiyo ni kweli kabisa. Na ninyi wanawake mtafanya jambo lile lile kwa waume zenu. Hiyo ni kweli.

354 Mara nyingine wanawake wanafikia mahali, ama . . .

355 Mwanamume anamwona maskini Yezebeli amejipodoa kweli kweli, mwajua, naye—naye ataenda kule, amtamani; labda ni mke mzuri. Kisha eti unajiita Mkristo. Aibu kwako. Unahitaji dozi nyingine ya madhabahuni. Hiyo ni kweli.

356 Na baadhi yenu—na baadhi yenu nyinyi wanawake mnatumbulia macho huku na huko kwa maskini jamaa fulani aliyelaza nywele zake nyuma, amezipaka vaselini ya kutosha kuweza kuufungua mdomo wake. Hata mnaninii . . .

357 Maskini msichana fulani, hapa si muda mrefu uliopita. Huu si utani, maana sitaki kulisema kama utani. Lakini watu wanajua ya kwamba hapa si mahali pa kufanyia mzaha. Lakini maskini msichana mmoja hapa, yeye . . . Kulikuwa na vijana wazuri hapa, wavulana Wakristo. Ni muda mrefu uliopita, wakati nilipokuwa mchungaji hapa, tulikuwa na mazoea ya kuwa na madarasa ya vijana wanaume tu. Nami ngingezungumza na vijana wanawake Jumapili alasiri, kuhusu jinsia na kadhalika. Halafu Jumapili iliyofuata alasiri, ninazungumza na vijana wanaume, na kujaribu kuyanyosha mambo hayo.

358 Maskini msichana mmoja akaanza kushikamana na maskini laghai fulani, mjini hapa, aliyevuta sigara na alikuwa na chupa mfukoni mwake. Naye aliendesha gari dogo wazi la watu wawili huku mjini. Sikuweza kuona kile alichooka katika mvulana huyo. Kijana huyo asingekuja kanisani. Angeketi huko nje. Anamleta msichana huyo hapa kanisani, na kisha huyo mvulana angeketi huko nje, kwenye gari lake, na kungojea, asingeingia kanisani. Nikamwambia msichana huyo siku moja. Aliishi huko New Albany. Nikasema, “Ninataka kukuuliza jambo fulani, wewe msichana. Ni kitu gani duniani hapa unachooka katika mvulana yule?” Nikasema, “Kwanza, yeye anachukia dini yenyewe u—ulio nayo. Anamdharau Kristo wako. Yeye kamwe hataweza kuwa mume mzuri kwako. Angekufanya uwe na maisha ya taabu, maishani mwako mwote.” Basi nikasema, “Vema, kuna wavulana wazuri Wakristo hapa ambao ungeweza kuambatana nao. Na kuhusu hilo baba yako na mama yako wanachukia wazo la wewe kuwa na mpenzi, hata hivyo unatoka nje tu, nawe unawazia, ‘Mimi ni kipusa anayevutia sana wa miaka kumi na sita.’”

359 Alianza kujipodoa na kutoroka, na muda si muda, alikuwa kwenye vilabu vya pombe. Ameenda Mbinguni sasa. Lakini, wakati huo, yeye alikuwa mfuasi wa hapa. Na mnajua ni sababu

gani huyo msichana alionipa nyakati zile, kwamba ni kwa nini alimpenda mvulana huyo? Alisema, “Ana miguu midogo miremba sana, na ananukia vizuri sana.” Ungeweza kuwazia jambo hilo? Akijiwekea uturi, huyo ni dondoadume, wala si mwanamume.

³⁶⁰ “Angalia,” nikasema, “dada, ni afadhali niambatane na mvulana Mkristo aliyekuwa na miguu kama ya magari ya changarawe na ananuka kama kicheche, kama huyo angalikuwa ni Mkristo kabisa.” Hiyo ni kweli. Kweli. Naam.

³⁶¹ Sababu yake aliyotoa ilikuwa, “Miguu midogo mizuri sana, na ananukia vizuri sana.” Maskini mtu anayezurura kwenye vilabu vya pombe, hatimaye aliyaangamiza maisha ya msichana huyo. Ni fedheha, aibu.

³⁶² Ndoa ni ya kuheshimiwa, bali inapaswa kuingiwa kwa maombi na kwa uchaji. Na upendo halisi kwa mwanamke huyo utawafunga pamoja milele. “Mtakachokifunga duniani, nitakifunga Mbinguni.” Unaposhuka kwenda huko mtaani, huenda akawa mzee na kuingia mvi na makunyanzi, bali upendo ule ule uliokuwa nao kwake wakati alipokuwa msichana mdogo, mwanamke mrembo, ungali utakuwa nao.

³⁶³ Unaweza ukainama mabega, ukapata upara, na kupata makunyanzi na cho chote kile, bali atakupenda kama tu mlivyopendana uliposimama ukiwa na mabega mapana na nywele za kipilipili, kama kweli ni Mungu. Kwa kuwa mnatazamia wakati mtakapovuka mto huko ng’ambo, wakati mtakaporudi ghafla tena, mwe vijana wanaume na wanawake tena, kuishi pamoja milele. Hiyo ni ahadi ya Mungu ya Milele. Yeye alisema atafanya jambo hilo. Yeye, si hivyo tu... tutalifikia mnamo dakika moja. Yeye aliapa ya kwamba angefanya hivyo.

³⁶⁴ Sikilizeni jambo hili, tunapoendelea.

Asiyekuwa kuhani kwa sheria ya amri... za jinsi ya mwili, bali kwa nguvu za uzima usio na ukomo.

³⁶⁵ Sasa tutasoma haraka; kusudi tuweze kulipata.

Maana ameshuhudiwa kwamba, Wewe u kuhani milele kwa mfano wa Melkizedeki.

Mradi kuhani atahitajika, Yeye atakuwa ni kuhani.

Maana, kuna ushahidi wa kubatiliwa kwa ile amri iliyotangulia... sababu ya udhaifu wake, na ya kutokufaa kwake;

Kwa maana ile sheria haikukamilisha neno,...

³⁶⁶ Huwezi, haidhuru ufanye nini. Unaacha kunywa pombe, unaacha kuvuta sigara, unakoma kusema uongo, unaenda kanisani na kujaribu kufanya hivi na kujaribu kufanya vile, ungali ni wa kimwili. Hiyo ni torati tu. Torati haikamilishi kitu chochote. Bali ni kitu gani kinachokamilisha? Kristo. Utukufu!

Huenda nikaacha kusema uongo, niache kuiba, nikaacha kufanya uzinzi, niache kutafuna tumbaku, niache mambo haya yote, na ningali wa kimwili. Mungu hapokei jambo hilo, kwa kuwa sina kitu cha kumtolea katika kipatanisho.

³⁶⁷ Lakini mara ninapoweka mikono yangu juu ya kichwa chenze baraka cha Bwana Yesu, na kusema, “Bwana, sifai kitu. Je! utanichukua kama mtumishi Wako?” basi Mungu anaiondolea mbali dhambi yangu kwa kunibusu, ninasimama mkamilifu mbele ya macho ya Mungu. Hiyo ni kweli. Kwa nini? Sitegemei ustahili wangu mwenyewe. Ninasimama juu ya Wake. Naye ametukamilisha, kwa kuteswa Kwake na Damu Yake.

³⁶⁸ Ninaona wakati wa kufunga umewadia. Bali nataka kumaliza kusoma hili nikiweza, upesi.

. . . iliyotangulia, kwa sababu ya udhaifu wake, na ya kutokufaa kwake.

(Kwa maana ile sheria haikukamilisha neno); na pamoja na hayo kulingizwa matumaini yaliyo mazuri zaidi, (Tumaini bora zaidi ni nini? Kristo.) ambayo kwa hayo twamkaribia Mungu.

³⁶⁹ Kwa nini? Katika wema wetu wote, na wema wetu wote, na wema wetu wote, tungali tu watu wa kimwili. Lakini mara tukiingia katika uwepo wa Mungu, tukitambua ya kwamba tusingeweza kusimama pale kamwe, ila tu kwa ustahilifu wa Yesu Kristo, basi tunamkaribia Mungu, kwa ustahilifu wa Mwanawe. “Bwana, ninakuja Kwako, kwa moyo usio na hatia. Katika Jina la Mwanao Yesu, nakusihi unipokee.” Loo, ndugu, ndipo unakuja kwa njia iliyo hai.

³⁷⁰ Sio, “Bwana, unajua niliacha kunywa pombe. Unajua ninamtendea mke wangu mema. Unajua ninafanya jambo *hili*. Ninafanya *lile*.” Huna kitu cha kutoa.

³⁷¹ “Kwa kuwa sheria iliyo ya jinsi ya amri za kimwili isingeweza kufanya kitu, bali kuingizwa kwa matumaini yaliyo mazuri zaidi kulifanya kitu. Tumaini hilo ambalo ni Kristo, tunalo kama nanga ya nafsi, iliyo imara na ya hakika.” Angalia.

Na kwa kuwa haikuwa pasipo kiapo . . .

Kiwakilishi nafsi, kama utaangalia hapa, kiko katika herufi za mlazo.

. . . yeye alifanywa kuhani;

Si kuhani tu, bali Yeye alifanywa kuhani kwa kiapo. Si . . .

³⁷² Sasa angalia. Hebu na tupate ukuhani huo mwingine.

(Maana wale makuhani, wale Walawi, ninii tu, watu wenye haki, waaminifu, wale makuhani walifanywa makuhani pasipo kiapo; . . .)

³⁷³ Mungu alisema tu, “Kwa mfano wa—kwa mfano wa Haruni, kwamba amewafanya makuhani hawa.” Walipita katika vizazi

mbalimbali, na wakaenda shuleni na kujifunza kuwa wahubiri na kadhalika. Walikuja. Kwa hiyo Mungu aliwafanya makuhani namna hiyo. Wao walijifanya makuhani, kwa elimu yao, kwa urithi wao, na kadhalika. “Bali Mtu huyu alifanywa kuhani kwa kiapo ambacho Mungu aliapa.” Sikilizeni kwa makini sasa.

(...walifanywa makuhani pasipo kiapo; bali yeye, pamoja na kiapo, kwa yeye aliyemwambia, Bwana ameapa wala hataghairi, amina, Wewe u kuhani milele kwa mfano wa Melkizedeki;)

Basi kwa kadiri hii Yesu amekuwa mdhamini wa agano lililo bora zaidi.

Sasa, upesi.

Tena wale walifanywa makuhani wengi, kwa sababu wazuliwa na mauti wasikae;

Maelfu mara maelfu mara maelfu, ya makuhani, kwa kuwa hawakuwa na kitu ila ni mauti na mauti tu na udhaifu, na mauti na mauti na mauti.

³⁷⁴ Bali mwangalie Yeye.

Bali yeye, (yeye ni nani?) Yesu, kwa kuwa daima akaa milele, anao ukuhani wake usioondoka. Ambapo...

Naye, kwa sababu hii, aweza kuwaokoa kabisa; haidhuru wako mbali vipi, jinsi walivyoinama, wako umbali gani, yeye anaweza kuwaokoa kabisa; wao wamjiao Mungu kwa yeye,...

Haikuwa kwa haki yako; bali kwa kukiri kwako. Unaona?

...wamjiao Mungu kwa yeye, maana yu hai sikuzote ili awaombe

Yeye yuko pale pale, sikuzote, akiwaombea.

Kutoka kwa kuhani mkuu wa namna hii aliyefanyika sisi, aliye mtakatifu, asiye kuwa na uovu, asiye kuwa na waa lolote, ametengwa na wakosaji, aliyefanywa kuhani mkuu mbinguni;

³⁷⁵ Hilo hapo. Sasa, kama nikijaribu kuwakilisha kesi yangu mwenyewe, nitashindwa. Kama nikijaribu kuwakilisha, niseme, “Vema, baba yangu alikuwa ni mtu mzuri. Baba yangu alikuwa mhubiri. Vema, nimeishi kanisani.” Bado nimeshindwa kesi. Lakini Mtu huyu ni Mkamilifu, Kristo. Yeye anaketi pale na kutoa dhabihu Damu Yake sikuzote kwa ajili ya dhambi zangu. Haya basi.

Ambaye hana haja kila siku, mfano wa...makuhani wakuu wengine, kwanza kutoa dhabihu kwa ajili ya dhambi zake mwenyewe, kisha kwa ajili ya dhambi za hao watu; maana yeye alifanya hivi mara moja, alipojitoa nafsi yake.

³⁷⁶ Sasa angalia kifungu cha mwisho.

Maana torati yawaweka wanadamu walio na unyonge kuwa makuhani wakuu; . . .

³⁷⁷ Hivyo ndivyo torati, torati ya kimwili, inavyofanya. Sasa, laiti ningalikuwa na kama saa mbili papa hapa. Hivyo ndivyo bado torati inavyowafanya wanaume kuwa wahubiri. Hiyo ni kweli.

³⁷⁸ Mbona, wao wanasema, “Vema, mtu huyu ana ujuzi wa seminari.” Nisingebadilisha tukio langu dogo la Mbinguni kwa seminari zote ulimwenguni.

³⁷⁹ “Mbona, tumemwelimisha mtu huyu. Yeye—yeye amechaguliwa kwa makini. Yeye ni mtu anayejiendeleza.” Sitaki kujiendeleza kwa namna hiyo. Ninapenda mtu anayeendelezwa na Mungu. Unaona? Unaona?

³⁸⁰ Lakini torati bado ingali inaweka makuhani. Torati bado ingali inaweka wahubiri. Ka—kanisa la Kibaptisti, wanasambaza wahubiri; chungu mbovu ya hao, wana mitambo inayowafyatua. Wamethodisti wanayo. Wabaptisti wanayo. Wapresbiteri, Wanazarayo, Wapilgrim Holiness, Wapentekoste, wanawafyatua haraka wawezavyo, kama mfumo mkubwa, mtambo mkubwa. Wanasimama pale kama ninii . . .

³⁸¹ Daima nilisema, “Kwa kweli ni—nilisikitikia kifaranga cha kuanguliwa kintambo.” Unajua, maskini kifaranga cha kuku kilichoanguliwa chini ya kiangulio, hakuanguliwa kwa njia ya kimaumbile asilia. La. Kuku ndiye anayepaswa kuangua kifaranga. Lakini kuku wa kiangulio, anapotoka nje, anasema tu “nywi, nywi, nywi,” wala hana mama wa kumwendea. Unaona? Yeye hajui mama ni kitu gani. Hiyo ni kweli. Yeye anaita mama, bali hana yeyote.

³⁸² Lakini maskini kifaranga aliyeanguliwa chini ya kuku, kwa njia asilia, yeye analia na mama anajibu. Hiyo ni kweli.

³⁸³ Na wakati mwingine ninafikiri juu ya ujuzi huu hapa wa seminari wa kutoka katika ninii, hivi viangulio vikubwa hapa Louisville na kote ulimwenguni, vikiangua wahubiri kwa maelfu. Viangulio vya Kipentekoste, na viangulio vya Kipresbiteri, na—na viangulio vya Kibaptisti, wote wanaangua vifaranga vya—vya—vyao wadogo. Wao wanafanya, “Nywi, nywi, nywi,” na kuzungumza juu ya kiangulio walimoanguliwa.

³⁸⁴ Bali mimi ninapenda kuwa na Baba, Mama. Jina la Bwana lihimidiwe! Si wengi waliozaliwa pamoja na mimi, bali wale waliokuwako walikuwa ni ndugu zangu. Amina. Tuna Mama anayejibu wakati unaninii . . . Mama aliye Mbinguni, anayetulea sisi sote. “Kama kuku anavyovifunika vifaranga vyake, na kuwanong’oneza, na—na kukibembeleza . . . kuvifunika vyake, vivyo hivyo nitawafunika ninyi. Loo, Yerusalemu, Yerusalemu, ni mara ngapi ningetaka kuwakusanya pamoja watoto wako kama vile kuku avikusanyavyo pamoja vifaranga vyake! Ni mara ngapi ningaliwafanya Wangu, bali hamkutaka.

Mlikuwa na semirari zenu wenyewe, mkawaangua makasisi wenu. Waliwafundisha dhidi Yangu. Sasa mmeachwa ukiwa. Maangamizi yenu yako mbele zenu.”

³⁸⁵ Ninasema jambo hili. Loo, enyi watu! Loo, enyi watu, ni mara ngapi Roho Mtakatifu angewakusanya, kama vile kuku avikusanyavyo vifaranga vyake! Bali mnataka njia yenu wenyewe. Mtataka mwe na njia yenu wenyewe kuhusu jambo Hilo.

³⁸⁶ Moja ya siku hizi usiku ningetaka kuhubiri juu ya, “Njia yako mwenyewe.” Mnajua, Kaini alitaka njia yake mwenyewe. Mwanadamu anataka njia yake mwenyewe, siku hizi. “Bali ipo njia inayoonekana kuwa sawa, bali mwisho wake ni mauti.”

³⁸⁷ Sasa angalia. “Katika jambo hilo Yeye anasema, ‘A—agano jipya...’” Ninaamini, sasa kwamba... La. Nilikuwa mahali pengine.

³⁸⁸ Kifungu cha 28.

Maana torati yawaweka wanadamu walio na unyonge kuwa makuhani wakuu; bali hilo neno la kiapo kilichokuja baada ya torati limeweka Mwana, ambaye amedumu hata milele.

³⁸⁹ Mungu ahimidiwe milele, juu ya Mwana aishiye milele kwa mfano wa Melkizedeki. Wala hakuwa na mwanzo. Wala kamwe hana mwisho. Wala torati haikuweza kutoa kitu kama hicho, kwa maana ilikuwa ni ya kimwili. Kanisa haliwezi kutoa kitu kama hicho, madhehebu, kwa maana ni ya kimwili. Se—seminari haziwezi kamwe kutoa kitu kama hicho. Walijaribu kuuelimisha ulimwengu kuliendea jambo Hilo. Walijaribu kuliundia madhehebu. Wamejaribu kila njia duniani, kufanya kila kitu ambacho wangeweza, na kuliacha jambo lenyewe muhimu: “Hamna budi kuzaliwa mara ya pili ndani Yake.” Mungu hukufanya ulivyo, hakika, si kwa sababu uliacha kufanya jambo *hili*.

³⁹⁰ Sasa, Wanazarayo, hamruhusiwi kuvaa pete, huwezi kuvaa saa, na inawabidi kuwa na vitu *fulani-fulani*, mikono yenu inapaswa kuwa mirefu namna *hii*, mikono ya vazi, sketi zenu zinapaswa kuwa ndefu *hivi*, nao nanii—nao wanaume hawawezi kuwa wanachama wa klabu. Nao hawatakubatiza kama hufanyi hivyo. Vema. Hawa hapa Wakatoliki wanaingia, nao wana mambo yao. Na hawa hapa Wamethodisti wanaingia, wana yao. Kila mmoja wao ana kipimo cha kupimia. Usipokifikia, vyema, huna chako. Unaona?

³⁹¹ Halafu basi, bali jambo lenyewe hasa ni, ni hili, “Sina kitu mkononi ninacholeta! Ninashikilia msalaba Wako tu. Ee Mungu, niko uchi, nimejeruhiwa, ninahitaji msaada. Loo, ninakuja kwa unyenyekevu kabisa, Kristo, nikikiri ya kwamba mimi si kitu wala hakuna kitu ndani yangu. Nipokee, Ee Mungu.” Ndipo Mungu anakupokea.

³⁹² Sasa, huenda hata usijue ABC zako. Huenda usitofautishe kati ya kahawa na maharagwe yaliyopasuliwa. Huenda ukajua, usitofautishe kati ya samli na siagi, mkono wa kulia na wa kushoto. Haijalishi ni kitu gani *usichojua*. Kuna jambo moja *unalopaswa* kujua, ya kwamba, Yesu Kristo alipachukua mahali pako wewe kama mwenye dhambi. Nawe unachukua mahali pako, kusimama katika haki Yake, ukikiri kila siku ya kwamba umekosea, na unampenda kwa moyo wako wote, na nia zako zote zimeelekezwa Kwake, utafaulu kwenda Mbinguni. Ni hayo tu, kwa kuwa Uzima uliokuwamo katika Kristo hauna budi kuwa ndani yako, la sivyo umepotea.

³⁹³ Kabla tu hatujafunga, je! mnakumbuka lile agano lisilo na masharti ambalo Mungu alifanya na Ibrahimu? Je! Yeye alifanya nini jioni hiyo wakati Mungu aliposema, “Hebu nione...” Wakati Ibrahimu aliposema, “Hebu nione jinsi utakavyofanya jambo hilo.” Mlango wa 16, nafikiri ndipo, wa Mwanzo. “Hebu nione jinsi utakavyofanya jambo hilo.”

³⁹⁴ Kasema, “Njoo hapa, Ibrahimu.” Ndipo akamchukua Ibrahimu, akasema, “Nenda ukaniletee ko—kondoo dume, na uende ukaniletee mbu—mbu—mbuzi, na uende ukaniletee ndama. Nami ninataka uwaletе hapa na ukatoe dhabihu.”

³⁹⁵ Ndipo Ibrahimu akaondoka akaenda na akampata kondoo, na mbu—mbuzi, na mwa—mwa—mwana-kondoo... ama ndama. Ndipo akawachinja. Wote walikuwa ni dhabihu safi. Kisha akawagawanya nusu katikati, kisha akawaanika. Halafu akaenda na akaleta hua wawili, na kuwaingiza ndani. Halafu Ibrahimu akawalinda ndege wasiwakaribie, akimngojea Mungu aje. “Sasa, Bwana, hiyo hapo dhabihu, utafanyaje jambo hili? Sijui jinsi utakavyoenda kumwokoa mwanadamu dhidi ya mapenzi yake mwenyewe. Sijui jinsi utakavyofanya jambo hili. Unawezaje kufanya jambo hilo, Bwana?”

³⁹⁶ Bwana akasema, “Sasa angalia, Ibrahimu. Wewe ni nabii. Wewe ni wa kiroho, nawe utafahamu ninayozungumzia.”

³⁹⁷ “Vema, Bwana, ninataka kuona.” Sasa ninalifanya kitamthilia.

³⁹⁸ “Kwa hiyo, Ibrahimu, njoo hapa sasa, na uketi chini hapa na uwalinde hao ndege.” Kwa hiyo akawafukuza ndege wote, mpaka jua lilipoanza kutua.

³⁹⁹ Na muda si muda wajua, Mungu akashuka. Aliposhuka, Ibrahimu alianza kushikwa na usingizi. Mungu akasema, “Ibrahimu, nitakupa usingizi.”

⁴⁰⁰ Sasa sikiliza, ewe rafiki mshika sheria. Unaona, Mungu alimwondoa Ibrahimu kabisa asihusike kwenye tukio hilo, hakuna kitu hata kidogo alichopaswa kufanya katika jambo hilo. Na hivyo ndivyo alivyokupata wewe. Ulisema, “Loo, nilimtafuta Mungu.” Hukumtafuta.

401 Mungu alikutafuta, “Hakuna mtu awezaye kunijia Mimi asipovutwa na Baba Yangu kwanza.” Unaona?

402 Ni Mungu akikutafuta, si wewe ukimtafuta Mungu. Wewe hukufanya hivyo hata kidogo. Asili yako ni mbaya. Wewe ni nguruwe. Hujui tofauti yo yote. Unaishi tu katika kizizi cha nguruwe. Hayo tu ndiyo unayojua. Unapenda jambo hilo. Unakunywa bia, unajichafua, unazurura na mke wa mtu mwingine, na ukifanya kila kitu kibaya unachoweza kufanya, inaonekana tu sawa. “Loo, ndugu, tuna wakati mzuri sana!” Unafikiri ni wakati mzuri.

403 Lakini Mungu anabisha hodi nafsini mwako. [Ndugu Branham anapigapiga mimbarani—Mh.] Hilo ndilo linalobadilisha. Si wewe ukibisha kwa Mungu; ni Mungu akibisha kwako. Adamu kamwe hakubisha kwenye moyo wa Mungu. Mungu alibisha kwenye moyo wa Adamu. Nawe u mwana wa Adamu. Hiyo ni kweli. Kabla Adamu hajawa mwana wa Mungu, tena, ilibidi Mungu abishe moyoni mwake. Kabla hujaweza kuwa mwana wa Mungu, Mungu hana budi kubisha moyoni mwako.

404 Ndipo, Ibrahimu akalala. Na wakati alipoingia usingizini, kitu gani cha kwanza alichooa? Giza kuu sana, la kutisha, la kuogofya. Hiyo ni mauti, inayoipata jamii nzima ya binadamu. Ndipo akaangalia mbele kidogo zaidi ya hapo, ndipo akaona tanuru iliyowaka moto. Kabla hujapata moshi, huna budi kuwa na moto. Hiyo ndiyo sababu ninaamini katika Jehanamu kama mahali panapowaka moto. Vema.

405 Yeye alionyesha, kila mmoja wetu hana budi kufa, na kila mmoja wetu anapaswa kwenda jahanamu, kwa kuwa sisi ni wenye dhambi.

406 Sasa, lakini, mbele zaidi ya hilo, aliona Nuru ndogo nyeupe.

407 Na Nuru hii ndogo nyeupe, Nuru hiyo ni nini? Nuru ile nyeupe ilikuwa ni nini? Ile Nguzo ya Moto iliyowatangulia wana wa Israeli. Nguzo ya Moto iliyokutana na Paulo akienda zake Dameski. Nguzo hiyo ya Moto iliyomtoa Petro gerezeni. Nguzo ya Moto iliyopo hapa usiku wa leo.

408 Yule Mungu wa Milele, adumuye milele, Yeye Mwenyewe alitembea katikati ya dhabihu hizi zilizopasuliwa, (loo, jamani), huku na huko kwenye kila moja ya hizo. “Hivi ndivyo nitakavyofanya jambo hilo, Ibrahimu. Hebu niangalie, nitakavyofanya. Ninafanya agano hapa. Nami nitaapa klapo, ya kwamba, kulingana na yule Mzao, nitamwinua Mwombezi. Nitafanya agano na mauti. Nami nitahukumu mauti, katika mwili wa nyama, kwa maana Mimi Mwenyewe nitakuja kufa. Ibrahimu,” akasema, “kupitia Mzao wako, Ibrahimu, nitakuja. Utakuwa baba wa ulimwengu, kupitia Mzao wako. Wala si wewe peke yako, ninayefanya naye ahadi, bali na Mzao wako baada yako.” Alijua kila mmoja atakayekuwa mzao wake. “Si wao;

bali ni kile ninachofanya. Nitalifanya, Ibrahimu. Nilimtumainia Adamu, naye akavunja lake. Na kila mmoja huvunja lao. Bali nitafanya hili na Nafsi Yangu, na kuapa kwa nafsi Yangu, ‘Nitalitimiza.’” Amina. Amina. Amina.

⁴⁰⁹ Tunafanya nini, tunapofanya agano? Ninasema, “Ndugu Neville...” Sasa angalia jambo hili, kwa dakika moja tu. Ninasema, “Ndugu Neville, hebu nikwambie nitakalofanya. Kama utahubiri mpaka... kesho usiku, na usiku ujao, uendelee mpaka Jumatano. Nitahubiri, kutoka Jumatano, na kuendelea mpaka Jumapili.” [Sehemu tupu kwenye kanda—Mh.] “Je! unafanya agano hilo?”

⁴¹⁰ “Naam, bwana.”

⁴¹¹ Hivi ndivyo tunavyolifanya. “Peana mikono, jamani.” [Ndugu Branham na Ndugu Neville wanapeana mikono—Mh.] Ndiyo hivyo. Hilo ndilo agano Marekani. Hivyo ndivyo tunavyofanya agano.

⁴¹² Sasa, wanafanyaje agano huko Japan? Tunafanya, tuseme, “Wewe fanya *hivi na vile*, nami nitafanya *hivi na vile*.” Tunachukua chumvi kidogo, maana chumvi ni ladha. Nasi tunachukua chumvi, nami ninaitupa juu ya Ndugu Neville, naye Ndugu Neville anachukua chumvi—chumvi na kuitupa juu yangu. Hilo ni agano la kudumu.

⁴¹³ Je! David Livingstone alifanyaje agano na yule mnegro wa Afrika, apate kuingia nchini mwake? Alienda na akaelewana na huyo chifu, kwamba aruhusiwe kupita kule, kuhubiri Injili nao wafanye kazi yao. Basi walichukua gilasi ya divai. Hili hapa agano na mnegro wa Afrika. Walichukua gilasi ya divai. Ndipo yule chifu mnegro akatoboa mishipa yake ya damu, akamimina hiyo damu kwenye gilasi hiyo ya divai. Naye David Livingstone akatoboa mishipa yake ya damu, akamimina damu hiyo kwenye hiyo gilasi ya divai. Wakaikoroga. Livingstone akanywa nusu yake, naye huyo chifu wa kingiro akanywa nusu yake. Kisha wakapeana zawadi, mmoja kwa mwingine, huyo chifu wa kingiro. David Livingstone akasema, “Unataka nikupe nini?”

⁴¹⁴ Akasema, “Koti hilo jeupe ulilovaa.” Kwa hiyo Livingstone akatoa koti lake akampa huyo chifu wa kingiro. Chifu akasema, “Unahitaji nini?”

⁴¹⁵ Akasema, “Huo mkuki wa heshima sana ulio nao mkononi mwako.” Maana, yeye alijua angeweza kuingia na huo, kwa hiyo akachukua mkuki huo. Nao walikuwa ni ndugu, kwa maana walifanya agano.

⁴¹⁶ Na alipokuwa akienda, na makabila hayo wangetoka mbio wapate kumwua, yeye aliinua mkuki huo wa heshima sana. Ndipo alipofanya hivyo, waliangalia na kusema, “Loo, loo, hatuwezi kumgusa mtu huyo.” Kwa nini? “Yeye ni ndugu wa agano, ingawa yeye ni mzungu, hatujawahi kumwona.”

Wao hawakujua walikuwa ni weusi mpaka walipomwona. Hawajawahi kuona mtu kama huyo maishani. “Lakini yeye ni ndugu wa agano. Ana mkuki wa chifu mkononi mwake.”

417 Ni picha nzuri namna gani, leo, ya kunywa agano la Damu ya Bwana Yesu, pamoja na nguvu za Roho Mtakatifu juu yetu! Tunasonga mbele katika Jina la Yesu, na ishara hizi zitafuatana na hao walio wake. Ni Mkuki mtakatifu wa Chifu. Unaona jinsi lilivyo, hilo agano?

418 Je! walilifanyaje katika zama za kimashariki? Waliapiana kiapo, mmoja kwa mwingine. Walimchinja mnyama, wakampasua, kisha wakasimama katikati yake kabisa. Hao—hao watu wawili walisimama katikati yake, huyo mnyama aliyepasuliwa. Ndipo wakafanya agano. “Nikishindwa kutimiza jambo *hili*, nikishindwa kufanya jambo *hili*, mbona, *hili* na *kadha* na *kadha*, mwili wangu na uwe kama wa mnyama huyu aliyekufa. Mwili wangu na uwe kama wa mnyama huyu aliyekufa.” Nao wanapofanya hivyo, wanachukua agano hili na kusimama katikati ya *hili*; wanakula kiapo, wanakula kiapo ya kwamba watalifanya. Nao wanararua karatasi, pamoja, vipande, na kumpa mtu mmoja kimoja, huyo mwingine hicho kingine. Kwenye wakati fulani watakutana. Na hebu na wafe kifo, wasipotimiza kiapo hicho; na wawe kama hao wanyama waliokufa. Vema.

419 Unawaona hao wanyama watatu? Wakamilifu; mwana-kondoo, mbuzi...na zile dhabihu tatu kamilifu. Mwana-kondoo aliainisha nini...Hua aliainisha nini? Na hao hua wawili walikuwa na maana gani? Hao hua wawili walitolewa sadaka kwa ajili ya wokovu na uponyaji pia, katika—katika ninii...iliyojumlishwa katika hiyo. Unaona? Upatanisho ulifanywa, tofauti, bali uponyaji uliendelea vivyo hivyo, na jinsi hiyo hiyo wokovu uliendelea vivyo hivyo. Wale hua wawili, wasiipasuliwa, ilimaanisha wamewakilisha, yote mawili. Wokovu... “Kwa mapigo yake tuliponywa. Alijeruhiwa kwa makosa yetu. Kwa mapigo yake sisi tuliponywa.” Waliwekwa upande mmoja, hawakutenganishwa. Lakini lile agano, ile sehemu ya mnyama huyo (wote watatu) ilipasuliwa. Unaona? Basi wakati walipofanya hilo, walirarua na kufanya agano lao.

420 Angalia vile Mungu alivyokuwa akimwambia Ibrahimu. “Pale Kalvari, pale Kalvari, kulingana na Mzao wako. Kutoka kwako alikuja Isaka. Kutoka kwa Isaka akaja *fulani*, Yakobo. Kutoka kwa Yakobo akaja Yusufu. Kutoka kwa Yusufu, na kuendelea, na kuendelea, na kuendelea, warithi, mpaka, hatimaye, kupitia kwa Mzao huyo mwenye haki!” Ninii yake...

421 Ndiyo kwanza amalizie, hapa, akisema ya kwamba Bwana wetu alitoka katika taifa lisilomjua Musa, hata kamwe hakunena habari zake. Lilitokana na ukuhani. “Bwana wetu alitoka katika kabila la Yuda.” Si kutoka kwa Lawi, kwa

kuwa wao walikuwa ni washika sheria wa kimwili. Bali Bwana wetu alitoka katika Yuda! Utukufu! Haya basi. Ambako ahadi ilifanywa!

⁴²² Sikilizeni kwa makini sasa, tunapofunga. Na pale Kalvari, Mungu alishuka na kuchukua mwili wa Mwanawe Mwenyewe, ambamo alikuwa ameishi, Naye akaupasua pale Kalvari. Kutokwa kwake na damu, akajeruhiwa, akatobolewa, na mkuki ulimchoma pale na kumrarua vipande, nayo Damu Yake ikabubujika. Ndipo akasema, “Baba, mikononi Mwako naiweka Roho Yangu.” Aliinamisha kichwa Chake. Ndipo dunia itikikisika, na vimulimuli vya radi vikamulika, na ngurumo zikanguruma. Mungu alikuwa akiandika agano Lake la milele.

⁴²³ Ndipo akatoa mwili wake uliokufa kutoka kaburini, kwenye siku ya kwanza ya juma, na akauleta juu Mbinguni, na akauweka pale kama Kuhani Mkuu, kama kumbukumbu; umeketi pale, mkamilifu, milele. Naye akamtuma Roho aliyemrarua kutoka katika mwili huo, moja kwa moja akamrudisha Kanisani. Na kanisa hilo halina budi kuwa na Roho yeye yule aliyekuwa katika mwili ule, la sivyo halitaungana Naye katika ufufuo. Vipande hivyo viwili havina budi kukamatana kikamilifu pamoja. Na kama Kanisa hili halina kwa utimilifu kabisa Roho yeye yule aliyekuwa katika Kristo, hutaingia kamwe kwenye Unyakuo.

⁴²⁴ Hilo hapo hilo agano la milele, ndugu. Litafute, wewe mwenyewe, kile kilicho moyoni mwako. Mpende Bwana. Uwe na hakika kabisa kwamba umeokolewa. Usibahatishe jambo hilo. Unabahatisha. Loo, wewe, sisi Wamarekani, tunapenda kucheza bahati nasibu, bali usibahatishe kwenye jambo Hilo. Uwe na hakika ya kwamba uko sahihi. Si kwa sababu eti ulijiunga na kanisa, bali kwa sababu kwamba kweli umezaliwa mara ya pili, Kristo ameingia ndani yako, katika Utu wa Roho Mtakatifu.

⁴²⁵ Sasa, kama tu maneno ya kuhitimisha, kuongezea, wakati nikifunga. Jinsi tunavyopaswa kuwa wenye furaha, kuona Roho yeye yule aliyekuwa katika Yesu Kristo, akiwa halisi miongoni mwa mtu kabisa, akifanya mambo yale yale aliyofanya wakati alipokuwa hapa duniani! Ni jinsi gani tunavyopaswa kuwa watu wenye furaha!

Hebu na tuombe sasa, tunapoinamisha vichwa vyetu.

⁴²⁶ Bwana, imekuwa ni siku muhimu. Ingawaje, ninajisikia kama vile ninavyojisikia sikuzote, nashindwa. Siwezi kulielezea vizuri, Bwana. Ninaomba ya kwamba utanisamehe kuhusu njia zangu za kijinga. Loo, ninatubu dhambi zangu mbele Zako, na kuomba rehema, nikijua ya kwamba kuna Kuhani Mkuu mashuhuri anayesimama huko ng'ambo kwenye mkono wa kuume wa Mungu, huko Mbinguni, ambaye hakufanywa kwa mfano wa Haruni, kwa kufuata torati na sheria na mambo kadha wa kadha. Lakini Yeye aliketi Pale kwa sababu ya neema

ya Mungu iliyoangalia mbele, kabla ya kuwekwa misingi ya ulimwengu, na kuniona mimi hapa chini ulimwenguni, na akafa kwa ajili ya dhambi zangu, apate kunirudisha kwenye Ufalme wa Mungu. Ninakushukuru Wewe, Baba, kwa ajili ya jambo hili.

427 Maana, Roho huyu ambaye sasa anatawala katika watu Wako ni wa Milele kama Mungu alivyo wa Milele. “Nawapa Uzima wa Milele, Uzima wa daima, Uzima wa milele, nao hawataangamia kamwe.” Na kwenye ile Hukumu, wao hawatakuwa huko kamwe. Wamepita tayari kwenye hukumu na wakaingia Utukufuni, “Na kama maskani iliyo ya dunia hii ikiharibiwa, tuna moja tayari inayotungoja huko ng’ambo kuingia.” Asante kwa ajili ya jambo hilo, Bwana.

428 Ninaomba sasa, kama akiwepo mmoja hapa, usiku wa leo, ambaye kabisa hajakunywa ile Damu halisi ya lile agano, ambaye hajui maana yake, hajui kuzaliwa mara ya pili ni kitu gani, kuwa na ushirika halisi pamoja na Kristo moyoni mwao, au moyoni mwa huyo mwanamke, jalia wampokee sasa hivi, tunapongojea na kutoa nafasi hii. Na kwenye Siku hiyo, tunaomba ya kwamba iwe tumeiwakilisha Injili katika Nuru halisi. Tunaomba, katika Jina la Kristo.

429 Huku tumeinamisha vichwa vyetu, je! kunaweza kuwe na mtu ambaye ungependa kumwinulia Kristo mikono yako, na kusema, “Kristo wa Mungu, unirehemu. Nijalie, kama mtumishi Wako asiyestahili, sasa nipokee Roho Mtakatifu moyoni mwangu. Na unipe hakikisho na upendo ninaohitaji hasa”? Kama huna Huo, Je! waweza tu kumwinulia mikono yako, ukisema, “Bwana, hii ni ishara ya kwamba ninataka jambo Hilo”? Je! ungeweza kumwinulia mkono wako? Mungu akubariki huko nyuma, bibi. Mungu akubariki hapa, bwana. Akubariki hapa, bwana. Mungu awe pamoja nawe. Hilo ni sawa. Mtu huyu hapa mwisho, Mungu akubariki, ndugu yangu. Mtu mwingine tena, kabla sasa hivi tu hatujafunga, tukiingojea tu kwa dakika chache. Mungu akubariki huko nyuma, mwanangu. Mtu mwingine?

430 “Sasa ninatamani. Ninatamani, Bwana Mungu. Unaujua moyo wangu. Unajua kilichoko niani mwangu. Wewe, “Roho wa Mungu ni mwepesi tena ni mkali kuliko upanga ukatao kuwili, hata kuvigawanya viungo na mafuta yaliyomo, na mtambuzi wa makusudi ya moyo.” Wazia jambo Hilo. Yeye anajua kabisa mawazo yako, nia yako.

431 Waweza kuinua mkono wako, useme, “Nirehemu, Mungu, sasa hivi. Ni—ninataka ujue ya kwamba ninajua ya kwamba nimekosa, na ninatambua jambo hilo, bali ninataka kuwa sahihi.” Vema, huku tunainamisha tu vichwa vyetu, tukiomba sasa, wazia tu muda kidogo. Hatutaki kuharakisha kuhusu jambo hilo.

Mwamba Wenye Imara
Kwako nitajificha!
Maji hayo na Damu
Yaliyotoka humu,
Hunisafi na dham. . .

Uponyaji maradufu! Yeye aliapa kwa jambo hilo, vitu viwili visivyoweza kubadilika.

Hunifanya mshindi.
Ninapovuta. . .

⁴³² Ee Bwana, tujalie sasa hivi kwamba sote tutatambua ya kwamba pumzi hizi tunazovuta zinapita. Hatujui tuna ngapi zaidi mbele zetu. Hayo yote ni kwa mashauri yako makuu. Ni jambo liamriwalo na Wewe. Loo, uturehemu. Na kwa wale walioinua mikono yao, Bwana, hakuna haja ya kuwataja. Unamjua kila mmoja wao. Lakini ninatoa tu ombi hili la maombezi kwa ajili yao. Ninaomba ya kwamba utaondoa hukumu kutoka katika moyo wao, na ujalie waje kwa ujasiri, sasa hivi, kwenye Kiti cha Enzi; watembe kwenda kwa ujasiri moja kwa moja hata kwenye Kiti cha Enzi cha Mungu, wakadai baraka zao walizopewa na Mungu. Uliwafanya wainue mikono yao. Wasingeweza kufanya jambo hilo kwa nafsi zao. Ninaomba, Mungu, ya kwamba utatujalia jambo hili katika Jina la Yesu. Amina.

. . . nitajificha!

Sasa, mwabuduni tu sasa.

Maji hayo na . . . (Loo, jamani!)
Yaliyotoka humu,
Hunisafi na dhambi,
Hunifanya mshindi.

⁴³³ Ni wangapi wanaojisikia vizuri sana sasa? Inua mkono wako, useme, “Bwana asifiwe!” [Kusanyiko linasema, “Bwana asifiwe!”—Mh.] Loo, Yeye ni mzuri sana! Loo!

Ipo Nafasi Kwenye Ile Chemchemi. Je! unaujua huo, Dada Gertie? Hebu tuninii. Ni wangapi wanaoupenda wimbo huo? Sasa tutakuwa na ibada ya ubatizo, katika muda mfupi tu ujao. [Ndugu Branham anazungumza na Ndugu Neville, “Je! utawabatiza?”—Mh.] Vema.

Nafasi, naam, nafasi ipo,
Ipo nafasi kwenye Chemchemi kwa ajili yako;
Nafasi, nafasi. . .

⁴³⁴ Vema. Hao wanaotaka ubatizo, wanaume wataenda kwenye chumba *hiki*, wanawake kwenye *hiki*, vema, hao watakaobatizwa katika Jina lililotukuka la Bwana wetu.

...mwema kwako,
 Ipo nafasi kwenye Chemchemi kwa ajili yako;
 Mungu amekuwa mwema sana kwangu,
 Ipo nafasi kwenye Chemchemi kwa ajili yako.

435 Kila mtu sasa.

Nafasi, nafasi, naam, nafasi ipo
 Ipo nafasi kwenye Chemchemi kwa ajili yako;
 Loo, nafasi, nafasi, naam, nafasi ipo,
 Ipo nafasi kwenye Chemchemi kwa ajili yako.

436 Loo, ninaupenda huo wimbo wa zamani. Ninyi je?

Ipo nafasi kwenye Chemchemi kwa ajili yako;
 Loo, nafasi, nafasi, ipo nafasi kubwa,
 Ipo nafasi kwenye Chemchemi.

437 Sasa, wakati mzee wa kanisa ameingia, kujiandaa kwa ubatizo, ningetaka kuwaelezea wasikilizaji. Nami nitawaomba baadhi ya mashemasi, kama wanaweza kunisikia humo chumbani, wakiwa tayari, waje na—na waniambie, ili kwamba tuweze kusogeza maikrofoni. Tunawataka ninyi nyote mwone jambo hili. Itachukua kama dakika kumi zaidi, ndipo kanisa litaruhusiwa liondoke.

438 Sasa ninataka kuwasomea baadhi ya Maandiko matakatifu. Ninataka kuyasoma kutoka katika Kitabu cha Matendo. Nami ninataka kuanzia kwenye kifungu cha 12 cha mlango wa 2 wa Matendo.

439 Sasa, ninataka mwangalie katika mlango wa 16 wa Luka Mtakatifu, ama wa Mathayo Mtakatifu, ninaamini ndipo lilipo, ya kwamba Yesu alikuwa akishuka kutoka mlimani. Wao... Akawaambia wanafunzi Wake, “Watu husema mimi Mwana wa Adamu ni nani?”

440 “Na baadhi yao walisema, mbona, Wewe ni ‘Eliya.’ Na wengine husema ya kwamba Wewe ni—Wewe ni ‘nabii yule.’ Na wengine husema ya kwamba Wewe ni *huyu* ama yule *mwingine*.”

441 Yeye akasema, “Lakini ninyi mnasema kwamba Mimi ni nani?”

442 Ndipo Petro akasema, “Wewe ni Kristo, Mwana wa Mungu aliye hai.” Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.]

443 Yesu akasema, “Heri wewe, Simoni Bar-yona kwa kuwa mwili na damu havikukufunulia hili. Hukulisoma hata kidogo kwenye katika seminari. Hukujifunza Hilo kupitia kwa mwanadamu.” Kasema, “Bali Baba Yangu aliye Mbinguni amekufunulia jambo hili. Nami nasema ya kwamba wewe ni Petro. Juu ya Mwamba huu nitalijenga Kanisa Langu. Milango ya kuzimu haitalishinda. Nami nakupa funguo za Ufalme wa Mbinguni.” Hiyo ni kweli? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] “Na lo lote utakalolifungua duniani, nitalifungua Mbinguni. Lo lote utakalolifunga duniani, nitalifunga Mbinguni.” Je!

Yeye alimaanisha jambo Hilo? Asingalilisema. Sasa, huku wakati ukisonga mbele—ulipokuwa unasonga mbele, sasa, Petro alikuwa na funguo za ule Ufalme.

444 Sasa, ninyi Wakatoliki, huenda mkafikiria hivi, ambapo kwamba mnasema, “Kanisa Katoliki limejengwa juu ya Petro.” Vema, tutaona. “Wao walikuwa na funguo. Kanisa Katoliki lingali lina hizo funguo.”

445 Hebu na tuone vile *Petro* alivyofanya kuhusu hizo funguo, unaona, ndipo tutapata kujua. Biblia ilisema, kwa Petro na kwa hao mitume wengine, “Enendeni ulimwenguni mwote. Wowote mtakaowaondolea dhambi, wameondolewa. Wowote mtakaowahesabia dhambi, wamehesabiwa.” Hilo, huenda nikalisema ili kwamba... Mtu fulani huenda asifahamu kile ninachomaanisha. Yesu aliwaambia wale mitume, “Wowote mtakaowasamehe dhambi, Mimi pia nitawasamehe. Na wowote msiowasamehe dhambi, na kuwahesabia hizo, Mimi pia nitawahesabia.” Hivyo ndivyo Yesu alivyosema.

446 Angalia kanisa Katoliki likijiingiza kwenye jambo hilo.

447 Lakini hebu na tuone jinsi walivyofanya jambo hilo. Basi kama tukiona jinsi walivyolifanya, basi inatupasa kulifanya vivyo hivyo. Sasa hebu tuone.

448 Ni siku ya Pentekoste. Kanisa linazinduliwa. Wote walikuwa katika chumba cha juu. Watu walitoka mle, wakinena katika lugha mbalimbali. Kwa nini? Kila lugha chini ya Mbingu iliwakilisha pale. Kiingereza kilikuwapo pale, pia. Kila lugha chini ya Mbingu ilipaswa kuwa pale, lugha yoyote iliyonenwa siku ile. Anaendelea hapa na kutoa lugha kadhaa, na jinsi ambavyo Wakrete na wageni, na waongofu wa Urumi, na—na—na Waarabu, na wote wanazungumza na kumtuku-... Sasa, hawakuwa wakisema katika lugha isiyojulikana. Walikuwa wakizungumza katika lugha zilizojulikana, kwa hao watu. Si lugha zisizojulikana, bali lugha ambazo kila mmoja alisikia. Mwenye dhambi, asiyeamini, aliweza kusikia yale aliyokuwa akisema. “Tunasikiaje katika lugha yetu wenyewe ambayo kwamba tu—tuliyojaliwa nayo?”

449 Sasa angalia. Sasa swali linakuja. Sasa, “Wengine walidhihaki.” Kifungu cha 12, vema.

*Wakashangaa wote wakaingiwa na shaka,
wakiambiana, Maana yake nini mambo haya?*

*Wengine walidhihaki, wakisema, Wamelewa kwa
mvinyo mpya.*

450 Walikuwa wakiwafanyia mzaha. Kwa sababu, walikuwa wakifanya nini? Walikuwa wakiyumbayumba kama walevi, kama walevi. Wakizungumza, bila kujua yale waliyokuwa wakisema, bali walikuwa wakihubiria kusanyiko hilo katika

lugha wao wenyewe wasizozijua, bali kusanyiko lilizijua. Unaona? Vema.

Wengine . . . wakisema, Wamelewa kwa mvinyo mpya, angalia vile wanavyofanya.

Wengine walidhihaki, wakisema, Hawa wamelewa . . .

“Bali Petro . . .” Angalia, jamani! Wewe ndiwe uliye na zile funguo.

Lakini Petro akasimama pamoja na wale kumi na mmoja, akapaza sauti yake, akawaambia, . . .

Sasa, kumbukeni, huku ni kuzinduliwa kwa Kanisa kwa mara ya kwanza.

. . . Enyi watu wa Uyahudi, na ninyi . . . mkaao Yerusalemu, lijueni jambo hili, mkasikilize maneno yangu.

Siryo mnavyodhani, watu hawa hawakulewa, kwa maana ni saa tatu ya mchana;

Vilabu vya pombe havikuwa hata vimefunguliwa wakati huo. Unaona?

Lakini jambo hili ni lile lililonenwa kwa kinywa cha nabii Yoeli,

Itakuwa siku za mwisho, asema Mungu, nitawamwagia watu wote Roho yangu, na wana . . . na binti zenu watatabiri; na vijana wenu wataona maono; na wazee wenu wataota ndoto.

Naam, na siku zile nitawamwagia watumishi wangu . . . na wanawake Roho yangu, . . . watatabiri.

Nami nitatoa ajabu katika mbingu juu, na ishara katika nchi chini; . . .

Sasa, ni Petro anayehubiri sasa, yule aliye na zile funguo.

. . . damu . . . moto, . . . na mivuke ya moshi.

Jua litageuka kuwa giza, . . . mwezi kuwa damu, kabla ya kuja ile siku ya Bwana iliyo kuu na iliyo dhahiri:

Na itakuwa kila atakayeliitia jina la Bwana ataokolewa.

Enyi waume wa Israeli, sikilizeni maneno haya; Yesu wa Nazareti, mtu aliyedhihirishwa kweni na Mungu kwa miujiza na ajabu na ishara, ambazo . . . alizifanya . . . kati yenu, kama ninyi wenyewe mnavyojua;

Nena kuhusu kukemea? Yeye alikuwa na zile funguo, mnajua. Ninii . . .

Mtu huyu alipotolewa kwa shauri la Mungu lililokusudiwa, na kwa kujua kwake tangu zamani, . . .

Haya basi. Yeye angeweza kutolewa? Kwa sababu Mungu alikusudia tangu mwanzo kuwa hivyo. Unaona? Kujua kwake Mungu tangu zamani!

⁴⁵¹ [Ndugu fulani anasema, kwa ajili ya ubatizo wa maji, "Tayari."—Mh.] Hebu kidogo tu. Waambie, wangojee kidogo tu, mpaka nitakapomaliza Maandiko.

. . . ninyi mkamsulibisha kwa mikono ya watu wabaya, mkamwua;

Ambaye Mungu alimfufua, akiufungua uchungu wa mauti kwa sababu haikuwezekana ashikwe nao.

Maana Daudi ataja habari zake, Nalimwona Bwana mbele yangu sikuzote, . . . yuko upande wa mkono wangu wa kuume, nisitikisike.

Kwa hiyo moyo wangu ukapendezewa, ulimi wangu ukafurahi, tena mwili wangu . . . utakaa katika matumaini.

Kwa maana hutaiacha roho yangu katika kuzimu; wala hutamtoa Mtakatifu wako aone uharibifu.

Umenijulisha njia za—zangu, njia zangu za uzima; utanijaza furaha kwa uso wako.

Waume, ndugu zangu, mniwie radhi, niseme kwa ujasiri mbele yenu habari za baba yetu mkuu, Daudi, . . . kuwa alifariki akazikwa, na kaburi lake liko kwetu . . . leo.

Basi kwa kuwa ni nabii, akijua ya kuwa Mungu amemwapia kwa kiapo, . . .

Ndiyo kwanza nimalizie kuhubiri jambo hilo.

. . . ya kwamba kulingana—kulingana na wazao wa viuno vyake, angeninii . . . katika uzao wa viuno vyake atamketisha Kristo katika kiti chake cha enzi;

Ni yale tu ambayo ndiyo kwanza nimalizie kuhubiri. Petro anahubiri jambo lile lile.

Yeye mwenyewe akitangulia kuyaona haya, nabii alitangulia kuyaona haya, alitaja habari za kufufuka kwake Kristo, ya kwamba roho yake haikuachwa kuzimu, wala mwili wake haukuona uharibifu.

Yesu huyo Mungu alimfufua, na sisi sote tu mashahidi wake.

Basi yeye, akiisha kupandishwa hata mkono wa kuume wa Mungu, kupandishwa mbinguni, . . . kupandishwa hata mkono wa kuume, kupandishwa mbinguni, akiisha kupokea kwa Baba . . . ahadi ya Roho Mtakatifu, amekimwaga kitu hiki mnachokiona sasa na kukisikia.

Maana Daudi hakupanda mbinguni, (yule nabii): bali yeye mwenyewe anasema, BWANA alimwambia Bwana wangu, Keti upande wa mkono wangu wa kuume.

Hata nitakapowaweka adui zako chini ya miguu yako.

Basi (sikilizeni jambo hili) nyumba yote ya Israeli na wajue hakika ya kwamba Mungu amemfanya Yesu huyu, yule mliyemsulibisha kuwa Bwana na Kristo.

Hilo linapaswa kutatua jambo hilo. Sivyo?

Walipoyasikia haya, hao wenye dhambi, wakachomwa mioyo yao, wakamwambia Petro . . . Waume . . . na Petro na . . . mitume wengine, Tutendeje, ndugu zetu?"

⁴⁵² Vema. Haya basi. Yeye ana nini? Ule ufunguo, ufunguo wa Ufalme huo. Ule Ufalme uko wapi? Umo ndani yenu. Hiyo ni kweli? Roho Mtakatifu ndiye Ufalme wa Mungu. Tunajua jambo hilo. Tunazaliwa kuwa katika ule Ufalme, kama raia na wajumbe. Angalia. Yeye ana ufunguo huo ubavuni mwake. "Utafanya nini nao?" Hii ndiyo mara ya kwanza huo mlango ulipowahi kufunguliwa.

⁴⁵³ Sasa, mhubiri anaulizwa swali, kwa mara ya kwanza, yule aliyekuwa na ufunguo. Ninaamini kama angalisema, "Simama kwa kichwa chako," hilo lingekuwa ni amri.

⁴⁵⁴ "Lo lote mtakalolifunga duniani, Mimi nitalifunga Mbinguni." Vema, "Lo lote usemalo, Mimi nitasema jambo lilo hilo. Wewe ndiwe uliye na ufunguo." Vema. Anaingiza ufunguo mlangoni.

. . . Unafanya nini? Tutendeje, ndugu zetu?

Walipoyasikia haya wakachomwa mioyo yao, wakamwambia . . . ndugu zetu?

Petro akawaambia, Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi yenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.

Kwa kuwa ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaotwa na Bwana Mungu wetu wamjie.

Hilo lililitatua milele. Hakuna watu kamwe, katika wakati wo wote, wangeweza kamwe, kamwe kupingana na Hilo.

⁴⁵⁵ Kanisa Katoliki lilikuja, badala ya kuzamishwa, wananyunyiza. Badala ya kuwa wanatumia Jina la Yesu, wakachukua, "Baba, Mwana, na Roho Mtakatifu." Hilo halijafundishwa kamwe katika Biblia.

⁴⁵⁶ Kila mtu, tangu wakati huo na kuendelea, alibatizwa kwa kuzamishwa katika Jina la Yesu Kristo. Na wengine walikuwa wamezamishwa na Yohana Mbatizaji, ambaye alimbatiza Yesu, Naye Paulo akawaambia wasingeweza kumpokea Roho Mtakatifu namna hiyo. Iliwabidi kurudi na kubatizwa tena,

tena, katika Jina la Yesu, kabla hawajaweza kumpokea Roho Mtakatifu. Ni wangapi wanaojua hayo ni Maandiko? [Kusanyiko linasema, “Amina.”—Mh.] Matendo, mlango wa 19. Haya basi. Maana, Ufalme wa Mbinguni ulifungwa kwa njia nyingine yo yote, kwa kiapo na Yesu Kristo, kwamba hilo lingekuwa ni amri rasmi Mbinguni.

... Tubuni mkabatizwe kila mmoja kwa jina lake Yesu Kristo, mpate ondoleo la dhambi zenu, nanyi mtapokea kipawa cha Roho Mtakatifu.

Sababu, ahadi hii ni kwa ajili yenu, na kwa watoto wenu, na kwa watu wote walio mbali, na kwa wote watakaotwa na Bwana Mungu wetu wamjie.

Amina. Na tuombe.

⁴⁵⁷ Baba, Mungu, usiku wa leo, miaka elfu moja mia tisa na kitu imepita, hata hivyo unyofu na uaminifu wa mioyo ya binadamu ingali inamlilia Mungu, kama iwavyo watoto wakililia maziwa ya titi la mama yao. Tunakupenda, Bwana. Hatuwezi kuishi bila ya Wewe. Kama vile Daudi alivyosema, “Nafsi yangu inakuonea kiu, kama ayala akioneavyo kiu kijito cha maji.” Hana budi kumpata, la sivyo atakufa.

⁴⁵⁸ Na, Baba, tumepitia katika Maandiko, huku na huko. Sio tupate kuwa tofauti, bali tunaona hizi seminari, wanafunzi wa theolojia siku hizi, ambao wanahubiri kulingana na amri za wanadamu, wala si amri za Mungu. Kwa hiyo, Bwana, hatuwadharau watu hao, bali tunayadharau mambo hayo wanayofundisha. Kwa hiyo, Bwana, tunaomba ya kwamba wawe ndugu zetu. Tunakuomba kwamba uwasamehe kosa lao. Nasi tunaomba ya kwamba watakuja kwenye Maandiko, wayasome, si vile baadhi ya seminari zinavyolifundisha, bali kulingana na vile ambavyo Mungu ameyaandika.

⁴⁵⁹ Tunaomba, Mungu, sasa, ya kwamba watu hawa wateule wanakuja usiku wa leo kwa ajili ya ubatizo wa maji. Wakati mchungaji wetu shujaa anapokuja kwenye mimbara hii na kutoka hapa, kuhubiri Injili, Injili ii hii; na halafu kwenda kwenye kidimbwi cha kubatizia, kuzika. Tujalie, Bwana, ya kwamba kila mmoja wa hawa atampokea Roho Mtakatifu, maana Wewe ulitoa ahadi, “Mtapokea Roho Mtakatifu.” Jalia Roho wa Mungu awe akiwangojea juu ya maji, kuwapokea wateule wa ubatizo usiku wa leo, kwa kuwa tunawakabidhi mikononi Mwako, katika Jina la Yesu Kristo. Amina.



KITABU CHA WAEBRANIA

Jumbe hizi kumi na moja za Ndugu William Marrion Branham zilizohubiriwa hapo awali katika Kiingereza kutoka tarehe 21 Agosti mpaka tarehe 22 Septemba, 1957, katika Maskani ya Branham huko Jeffersonville, Indiana, U.S.A., zimetolewa kwenye kanda za sumaku zilizorekodiwa na kuchapishwa bila kufupishwa katika Kiingereza. Tafsiri hii ya Kiswahili ilichapishwa na kusambazwa na Voice of God Recordings. Ilichapishwa tena katika mwaka wa 2013.

SWAHILI

©2009 VGR, ALL RIGHTS RESERVED

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org

Ilani ya haki ya kunakili

Haki zote zimehifadhiwa. Kitabu hiki kinaweza kuchapishwa kwa matbaa ya nyumbani kwa matumizi ya kibinafsi ama kusambaza, bila malipo, kama chombo cha kuitangazia Injili ya Yesu Kristo. Kitabu hiki hakiwezi kikauzwa, kunakiliwa kwa wingi, kuwekwa kwenye mtandao, kuhifadhiwa kikatolewe tena, kufasiriwa katika lugha zingine ama kutumiwa kuomba fedha bila idhini halisi iliyoandikwa moja kwa moja kutoka Voice Of God Recordings®.

Kwa habari zaidi ama kwa vifaa zaidi, tafadhali wasiliana na:

VOICE OF GOD RECORDINGS
P.O. Box 950, JEFFERSONVILLE, INDIANA 47131 U.S.A.
www.branham.org